Gazeti la kwanza la Kiislam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

# Mapenzi ya Mungu

DAR ES SALAAM TANZANIA

JUZU 73 No. 168 | JUMADIUL-AWWAL1433AH | MEI 2012 | HIJRAT 1391 HS | BEI TSH. 500/=

**Nukuu ya Qur'an Tukufu**

Na ikiwa makundi mawili katika waaminio wanapigana, basi fanyeni suluhu kati yao; na ikiwa moja la hayo limemrukia mwenziwe, basi lipigeni lile lililorukia mpaka lirudie kwenye amri ya Mwenyezi Mungu. Na kama likirudi, basi yapatanisheni baina yao kwa uadilifu, na hukumuni kwa haki. Hakika Mwenyezi Mungu Huwapenda wanaohukumu kwa haki. ***(Al-Hujraat 49:10-).***

# Kiongozi wa waaminio duniani aonya: Israel acha ubabe na ukandamizaji

Taifa la Israel ambalo lilianzishwa mwaka 1948 kutokana na tamko la Balfour limeendelea kuwa mwiba wa kisiasa huko Mashariki ya Kati. Limeteka baadhi ya ardhi za Waarabu na kuendelea kuwabughudhi na kuwatia mashaka makubwa Wapalestina. Kwa hivi sasa wanao mpango wa kushambulia taifa la Iran.

Hatua hii ni hatari kwa amani ya dunia. Ni katika muktadha huu ndipo Kiongozi wa Ahmadiyya duniani akatoa onyo kali kwa Israel. Ifuatayo ni barua



aliyomuandikia Waziri Mkuu wa Israel Benjamin NetanyaHu

Mheshimiwa, Bw. Benjamin Netanyahu, Waziri Mkuu wa Israel, Jerusalem.

Mpendwa Waziri Mkuu,

Hivi karibuni nilituma barua kwa Mheshimiwa Shimon Peres, Raisi wa Israel, kuhusiana na hali yenye hatari inayoibuka duniani. Kutokana na hali zinavyobadilika kwa kasi, niliona yanipasa pia nikutumie ujumbe wangu,

*Endelea uk. 2*

# Islam inadhamini amani ya dunia - Amir Sahib

Tarehe 20/4/2012 katika ukumbi wa hoteli ya Peacock, Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya nchini iliwakaribisha wapenda amani kutoka taasisi za kiserikali, kidini na kijamii ili kulizungumzia swala hili katika ulimwengu wetu huu. Amir Mbashiri Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya nchini Sheikh tahir Mahmood Chaudhry alitoa ufafanuzi wa Islam imetumia njia zipi katika kuleta amani miongoni mwa wanadini. ifuatayo ni hotuba ya ufafanuzi huo.

Ndugu waheshimiwa!

Assalaam Alaikum warahmatullah wabarakaatuh.

Miaka elfu moja na mia tano iliyopita, Mwenyezi Mungu Alimtuma Mtume Muhammad s.a.w. kuja kukamilisha jengo la kiroho la kustawisha amani na upendo duniani. Mitume




***Amir na Mbashiri Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Tanzania Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry akitoa hotuba katika mkutano wa amani uliofanyika tarehe 20 April 2012 katika ukumbi wa hoteli ya Peacock jijini Dar es Salaam***

wote waliopita kabla yake waliifanya kazi hii adhimu na kubakisha sehemu fulani iliyokuja kamilishwa na Mtume wetu Muhammad s.a.w., kama vile mwenyewe alivyosema kuwa mfano wake na manabii waliopita, ni sawa na jengo moja zuri sana ambalo kila mtu alikuwa akilisifia kwa uzuri na shani yake, lakini kila mtu akawa anatamani, laiti ile

*Endelea uk. 3*

# Hakika ya tukio la Msalaba

**Na Mwl. Abdullah H. Mbanga**

Katika aya 4:158 - 159 ya Qur'an Tukufu kumetajwa tukio la msalaba. Tukio linalohusiana na maisha ya Nabii Isa bin Mariyam (as), Nabii wa Kiisraeli aliyeishi zaidi ya miaka 2000 iliyopita. Aya hii inakataa waziwazi ya kuwa Nabii Isa bin Mariyam (as) hakuuawa wala hakusulubiwa isipokuwa alifananishwa kwao.

Kusudi la makala hii ni kutoa ufafanuzi juu ya mkanganyiko mkubwa uliojitokeza hususan miongoni mwa Waislam kuhusiana na kadhia nzima ya tukio la msalaba.

Ingawa aya haisemi kuwa Yesu hakuwambwa Msalabani, lakini kuna baadhi ya Waislam wanaodai kuwa Nabii Isa (as) hakuwahi kukamatwa wala kuwekwa msalabani, bali alipaishwa mbinguni na badala yake mtu mwingine alikamatwa, akateswa na kusulubishwa badala yake. Dhana hii inatokana na kufuata maana potofu ya neno 'SWALABU' wakimaanisha kuwa ni kumfunga mtu mtini.

Ni kweli ya kwamba aya imetumia maneno mawili ya kiarabu 'QATALA' na 'SWALABA'. Ukweli ni kwamba neno 'QATALA' humaanisha kuua tu, bila kutumia adhabu maalum. Neno 'SWALABA' humaanisha adhabu maalum ya kifo. Kusulubisha ni adhabu ya kidesturi ya kuwaua wakosefu tangu kale katika jamii ya watu wa Misri. Adhabu hii ilitumiwa sana na Mafirauni katika kukomesha uasi dhidi ya Serikali zao tangu zama za Nabii Musa (as) (Qur'an 7:125). Bali uwepo wa adhabu ya aina hii unaonekana kuwepo tangu zama za Nabii Yusuf (as) ambaye aliishi Misri. Inasomeka ndani ya Qur'an Tukufu (12:49) Nabii Yusuf (as) alimtabiria Mfungwa mwenzake kwamba atasulubishwa hadi ndege

*Endelea uk. 4*

# Mapenzi ya Mungu

## Maoni ya Mhariri

## Demokrasi yaenda wapi?

**Habari za kuaminika kutoka kwenye vyanzo vyetu vya kuaminika, ni kuwa kwa muda sasa jeshi la Marekani kubwa kuliko yote duniani kwa kuhodhi silaha limekuwa likiwafundisha wanajeshi wake kuichukia dini tukufu ya Islam mahala pake patakatifu mila za kiislam na Waislam wenyewe kwa ujumla.**

**Hatuelewi vizuri chuki hii imechumbukana na nini? Jambo hili linastua kwa sababu kwa miaka mingi serikali ya Marekani chini ya mwamvuli wa vita baridi ilikuwa inapinga jamii zote zilizokuwa haziheshimu uhuru wa kuabudu. Jamii zilizotangaza kadamnasi kwamba Mwenyezi Mungu (Mungu Apishe mbali) Hayupo. Ni huzuni kubwa kuona taifa kubwa na tajiri duniani likitumbukia katika shimo hilo la chuki za kidini wakati tangazo lao la uhuru la mwaka 1776 linaeleza kinaga ubaga juu ya utukufu wa kuruhusu watu kuwa na uhuru wa kuabudu na bila kudharau imani ya mtu yeyote yule.**

**Marekani isianze kuchafuliwa kwa sasa. Taifa hilo lilianzishwa kwenye misingi ya uhuru, uhuru wa kuabudu na uhuru wa kutafuta. Ni taifa linaloendelea kuwapokea watu wote ambao wanatafuta maisha bora na ni jamii inayoongozwa na wazo la Abraham Lincoln lisemalo 'Serikali ya watu kwa ajili ya watu'. Taifa ambalo mpiganaji mashuhuri Martin Luther King aliweza kuwa na njozi kuwa siku moja Mmarekani hatahukumiwa kutokana na rangi yake bali kutokana na khulka yake.**

**Ni uonevu mkubwa kuionea dini tukufu ya Islam. Hii ni dini ya amani. Hii ni dini ya mapenzi na huruma. Maisha ya Mtukufu Mtume Muhammad (saw) ni kitabu kilicho wazi. Aliishi na watu wa kila aina bila ya ubaguzi wala chuki. Na hakuna mwakilishi bora wa Islam isipokuwa Mtukufu Mtume Muhammad (saw). Tunajiuliza huyo anayefundisha wanajeshi wa Marekani juu ya Uislam anafahamu kwa kiasi gani mafundisho ya dini hii tukufu?**

**Wamerekani kama kuna kazi kubwa inayowasubiri kwa hivi sasa ni kusoma tena kwa tamakuni maisha ya Mtukufu Mtume Muhammad (saw) kwa sababu katika maisha yake kuna dawa ya kutibu maradhi ambayo yametapakaa Marekani na duiani kote.**

**Hapana shaka Islam imeweka mipaka katika kila kitu na inasisitiza daima kufuata njia ya kati, maarufu kama 'Wastwa'. Lazima pawepo na mipaka katika nyanja zote za maisha. Uhuru kwa mathalani ni jambo jema lakini bila shaka lina mipaka. Unaweza kuubembeza mkono kadri unavyotaka lakini uhuru wako unaishia pale mkono wako unapogusa pua yangu.**

**Inasemekana kwamba tamko la Rais Obama la kuunga mkono mahusiano ya ndoa ya watu wa jinsia moja ni sehemu ya Demokrasia ya nchi hiyo ya Marekani. Tunajiuliza je hiyo ni moja ya harakati za kupata urais wa muhula wa pili? Je hakuna haja ya kutazama njia unayotumia ili kufikia kwenye shabaha yako? Je haoni ya kwamba historia itaweka doa katika urais wake? Ni uhuru gani huo unaovunja mizizi ya jamii. Ni uhuru gani huo unaovunja miti ya jamii? Mti wa uhuru wa Amerika utaotaje wakati mizizi yake imeoza. Au tuseme sasa Marekani imefikia mwisho wa safari yake? Kwani historia ya dunia inatuonyesha kuna kujaa na kupwa katika historia ya mataifa yote. Katika hali hiyo tunawakumbusha Wamerekani maneno ya Allah; "Tembeeni katika ardhi muone ulikuwaje mwisho wa wale waliokadhibisha"**


**BODI YA UHARIRI**

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Mahmood Hamsin Mubiru.
Kompyuta: Abdurahman M. Ame.
Mchapishaji: Sheikh Muhammad Arif
Msambazaji: Mwl. Omar Mnungu
Wajumbe: 1. Abdullah Khamis Mbanga
2. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu@yahoo.com


# Kiongozi wa waaminio duniani aionya Israel

*Kutoka uk. 1*

kutokana na kuwa kwako mkuu wa serikali ya nchi yako.

Historia ya nchi yako imeshikamana kwa karibu sana na bishara na ufunuo wa Mwenyezi Mungu. Kwa hakika manabi wa wana wa Israeli walitoa bishara za uwazi kabisa kuhusiana na mustakbali wa Taifa lako. Matokeo ya kuyaasi mafundisho ya manabii na kughafilika na bishara zao, wana wa Israeli wakalazimika kupata shida na mateso. Kama viongozi wa Taifa lako wangekuwa imara katika kuwatii manabii, wangeokolewa na shida na balaa zilizoendelea kuwashukia. Hivyo, ni jukumu lako, pengine kwa sasa zaidi kuliko wengine, kuzizingatia bishara na maagizo ya manabii.

Nakuambia haya nikiwa kama Khalifa wa Masihi na Imam Mahdi yule Aliyeahidiwaa.s.aliyetumwa kama mtumishi wa Mtume mtukufu Muhammad s.a.w. na Mtume (huyo) Mtukufu s.a.w. alitumwa kuwa rehema kwa wanadamu wote akitokana na ndugu za wana wa Israeli akifanana na Musa a.s. (Kumbukumbu la Taurati 18:18). Hivyo ni jukumu langu kukukumbusha ujumbe wa Mwenyezi Mungu. Natumai kwamba utakuja hesabiwa kuwa miongoni mwa wale wenye kuuitikia mwito wa Mwenyezi Mungu na kufanikiwa kuitafuta njia iliyo sahihi, njia ile inayoafikiana na mwongozo wa Mwenyezi Mungu, Aliye Bwana wa Mbingu na Ardhi.

Twasikia taarifa siku hizi, ndani ya vyombo vya habari, kuwa wajiandaa kuishambulia Iran. Juu ya hayo matokeo yenye kutisha ya vita vya dunia yako mbele yako. Katika vita vya dunia vilivyopita, wakati ambapo mamilioni ya watu wengine walikufa, maisha ya malaki ya wayahudi pia yalipotezwa. Kwa kuwa kwako Waziri Mkuu, ni jukumu lako kulinda uhai wa Taifa lako. Mazingira ya sasa ya dunia yadhihirisha kwamba vita ya dunia haitapiganwa na nchi mbili pekee, bali makundi (ya nchi zenye kuhasimiana) yataibuka. Tishio la kutokea kwa vita kuu ya tatu ni kubwa sana. Maisha ya Waisalam, Wakristo na Wayahudi yako hatarini kutokana nalo. Endapo vita kama hiyo itatokea itazua mmenyuko mfulizo (chain reaction) wa mauwaji ya wanadamu. Matokeo ya balaa hili yatawafika vizazi vijavyo, ambao aidha watazaliwa na mapungufu mbalimbali au na ulemavu wa viungo. Hii ni kwa sababu bila shaka vita kama hiyo itahushisha matumizi ya silaha za maangamizi.

Hivyo, ni ombi langu kwako kwamba badala ya kuipelekea dunia kwenye shiko la vita, fanya juhudi kubwa iwezekanayo kuinusuru dunia na janga hili. Badala ya kutatua migogoro kwa mabavu, jaribu kuitatua kwa njia ya mazungumzo ili tuweze kuvizawadia vizazi vijavyo hatima angavu badala ya kuvizawadia mapungufu na ulemavu.

Nitajaribu kuelezea maoni yangu kwa kutumia mafundisho yenu, nukuu ya kwanza ikiwa ni ya Zabur:

"Usikasirike kwa sababu ya watenda mabaya, Usiwahusudu wafanyao ubatili. Maana kama majani watakatika mara, Kama miche mibichi watanyauka. Umtumaini BWANA ukatende mema, Ukae katika upendezwe nauaminifu. Nawe utajifurahisha kwa BWANA, Naye takupa haja za moyo wako. Umkabidhi BWANA njia yako, Pia Umtumaini naye atafanya. Ataitokeza haki yako kama nuru, na hukumu yako kama adhuhuri. Ukae kimya mbele ya BWANA, Nawe umngojee kwa saburi. Usimkasirikie yeye afanikiwaye katika njia yake, wala mtu afanyae hila. Ukomeshe hasira, uache ghadhabu, Usikasirike, mwisho wake ni kutenda mabaya. Maana watenda mabaya wataharikiwa, Bali wamngojao BWANA ndio watakaoirithi inchi. Maana bado kitambo kidogo asiye haki hatakuwapo, Utapaangalia mahali pake wala hatakuwapo. Bali wenye upole watairithi inchi, Watajifurahisha kwa wingi wa amani." (Zabur 37. 1-11)

Kadhalika tunakuta kwenye Torati:

Usiwe na mawe ya kupimia mbalimbali, kubwa na dogo, katika mfuko wako. Usiwe na vipimo mbalimbali kikubwa na kidogo, katika nyumba yako. Usiwe na jiwe timilifu la haki uwe na kipimo timilifu cha haki, zipate kuwa nyingi siku zako, katika nchi akupayo BWANA, Mungu wako. Kwa kuwa wote wayatendao mambo kama haya, wote watendao yasiyo haki, ni machukizo kwa BWANA, Mungu wako. (Kumb. 25. 13-16)

Hivyo, viongozi wa ulimwengu hususan wewe, wapashwa kuacha kuendesha serikali kwa mabavu na kuacha kuwakandamiza wanyonge. Badala yake wadumu kueneza na kuhamasisha haki na amani. Kwa kufanya hivyo nyinyi wenyewe pia mtakuwa kwenye amani, nguvu zenu zitaongezeka na amani ya dunia itapatikana.

Ni maombi yangu kwamba wewe na viongozi wa dunia watauelewa ujumbe wangu, na mtalitambua daraja lenu na hadhi yenu, na kutimiza wajibu wenu.

Wenu Mwaminifu,

**MIRZA MASROOR AHMAD**
Khalifatul Masih V *Kiongozi Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya Duniani.*

**Tafsiri: DAWATI LA KISWAHILI,**
**S. L. P. 1,**
**MOROGORO,**
**TANZANIA.**

# Islam inadhamini amani ya dunia

*Kutoka uk. 1*

sehemu ya tofali iliyopungua ingekamilika, ili kukamilisha uzuri na shani yake. Hivyo akasema kwamba yeye, yaani Mtume s.a.w., ndiye tofali lile lililosalia na hivyo kulifanya jengo hilo kuwa na uzuri na shani iliyokamilika. Akapewa sheria iliyokusanya sheria zote walizopewa manabii waliopita ambazo Mungu Alidhamiria ziendelee kutumika kwa wanadamu daima dawamu jinsi zilivyokuwa au kwa marekebisho kadhaa.

Hapa nitatoa mfano mmoja tu wa kuonyesha jinsi Mtume Muhammad s.a.w. alivyokuja kuyakamilisha au kuyaboresha mafundisho ya manabii waliopita kabla, na pengine kuyasahihisha pale ilipotokea kwamba wafuasi wa mafundisho hayo wameyaharibu baada ya kifo cha nabii wao.

Nabii Musa a.s. aliwaamuru wafuasi wake waliokuwa wameathirika na tabia ya woga na unyonge, uliosababishwa na kukaa kwao utumwani kwa karne kadhaa, wajilipize kisasi kwa wale waliokuwa wakiwadhulumu haki zao za kibinadamu, ili wajenge tabia ya ujasiri wa kukataa kudhulumiwa. Kwa hiyo wakapewa sheria ya jino kwa jino na jicho kwa jicho. Lakini hata hivyo wakapewa pia agizo la kusamehe, ingawa mkazo uliwekwa zaidi kwenye agizo la kisasi, ili wasije tu kusamehe kutokana na woga uliokithiri ndani ya silika zao kutokana na kukaa utumwani kwa karne nyingi.

Walipodumu kwa miaka kadhaa ndani ya sheria hiyo, zikafika zama ambapo, Ibilisi, kama ilivyo desturi yake, akawatelezesha wana wa Israeli na hivyo wakaamua kujifanyia marekebisho ya sheria waliopewa na Mwenyezi Mungu kupitia nabii Musa a.s., na hivyo kuamua kukifuta kipengele kile cha sheria kilichoagiza kusamehe. Wakati huo mioyo yao ilikuwa tayari imejasirika na kupita kiasi katika ujasiri, na hivyo wakaona hakuna haja tena ya kusamehe.

Hawakuishia hapo, bali hata sheria ya kisasi ikaongezewa makali, na hivyo kiutendaji, wakawa wanalipiza jino kwa meno na jicho kwa macho. Hali hii ikakithiri sana na manabii wengi wakatumwa kwao ili kuja kuirekebisha hali hii iliyokuwa kikwazo kikubwa cha amani. Mitume hao walifanikiwa kwa kiasi fulani kurekebisha mambo, na hatimaye hali ilipokithiri kwa uovu na kusababisha wana wa Israeli kugawanyika ndani ya makundi sabini na mbili yaliyohasimiana, na kutowesha kabisa hali ya utulivu na amani, na kusababisha wawe tena dhaifu na wanyonge na hivyo kutoa mwanya wa kuwekwa tena utumwani na taifa la kizungu la Kirumi, ndipo huruma ya Mwenyezi Mungu ikawateremkia tena kwa kutumiwa nabii wa daraja la juu kabisa aliyetokea ndani ya umati wao kwa dhati ya nabii Isa a.s. au Yesu, kama anavyotambulika na ndugu zetu wapenzi wakristo.

Nabii huyu akaagizwa kukabiliana na chanzo chenyewe kilichosababisha kutoweka kwa amani, ambacho ni wana wa Israeli kuyaepuka baadhi ya mafundisho ya asili ya Taurati kwa kuyafuta baadhi na kuyapindisha baadhi. Kwa hiyo Yesu akaagizwa ayasisitize sana mafundisho ya Taurati yaliyofutwa na Wayahudi ya kusamehe, bila ya kuyaondoa mafundisho ya kisasi ya jicho kwa jicho, kama mwenyewe alivyosema kuwa hakuja kuyabadili mafundisho ya Taurati na manabii bali kuyatimiliza, yaani kuyarudisha katika hali yake kamili ya asili kama yalivyoteremshwa kwa nabii Musa a.s. na kusisitizwa na manabii wengine waliokuja baadae kati yao.

Ndipo alipofundisha kuwa mtu akikuzaba kibao kwenye shavu moja basi mgeuzie pia na shavu la pili. Hili ni fundisho lililosisitiza silika ya kusamehe ambayo Wayahudi walilazimika wawe nayo ili kukabiliana na ushupavu uliokwisha jengeka ndani ya mioyo yao iliyobadilika na kuwa sugu. Fundisho hili likawageuza Wayahudi waliomkubali na kumpokea Yesu, wakawa tena watu rahimu na wapole, na hivyo ikawa rahisi kwao kupanda katika daraja za juu za ucha Mungu. Mapinduzi hayo yakawakaribishia upendo na msaada makhsus wa Mwenyezi Mungu na hivyo wakawezeshwa kuitawala tena sehemu kubwa ya dunia na kufanikiwa kuondoa maovu na ujahili mkubwa katika mataifa waliyoyashinda na kuyateka na hivyo kustawisha amani kwa msingi wa mafundisho ya kimbingu.

Baadae, kama kawaida yake, Ibilisi akafanikiwa tena kujipenyeza na kusababisha watu hao waanze tena kuyabadili mafundisho matakatifu. Mabadiliko yakawa ni mengi na ya kutisha mno kiasi ya kwamba Mwenyezi Mungu Akaamua kuleta sheria mpya iliyojenga msingi kwenye sheria za manabii waliopita kwa watu na zama tofauti. Mtume Muhammad s.a.w. akateuliwa kuileta sheria hiyo duniani na ndio sheria iliyounda dini ya Islam, dini iliyojengwa kwa hatua na manabii wote wa Mwenyezi Mungu, akiwemo Adam, Nuhu, Ibrahim, Musa, Isa na kadhalika.

Mtume Muhammad s.a.w. akawakuta wayahudi wamegawanyika katika makundi mawili. Wale waliomkataa Nabii Isa a.s. wakawa wameshikilia ushupavu wao, na wale waliomkubali Nabii Isa a.s. ambao, nao pia ikawawia vigumu kulishikilia fundisho hilo la kusamehe kutokana na baadhi ya wasamehewa kuendeleza utukutu badala ya kujirekebisha. Ndipo Mtume s.a.w. akaja na fundisho lililokuwabainayamafundisho hayo yaliyopita kiasi na kuelemea upande mmoja. Yaani mlipizie kisasi yule aliyekukosea kwa kiwango kile kile alichokukosea, lakini umsamehe pale uonapo kuwa msamaha ule utamhuzunisha na kumfanya ajirudi na kutubia kosa lake. Na kama silika yake ni ya ushupavu ya kutojirudi basi adhabu kwake kwa njia ya kisasi ndio wajibu wake anaostahili kuupata kwa kiwango kile kile alichokudhuru.

Wastani huu ulisaidia sana kuwadhibiti wakosefu wavunjao amani na hatimae mipango madhubuti ikaendelea kufunuliwa kwa Mtume s.a.w., likiwemo agizo la kuwatii viongozi wa serikali yoyote iliyopo madarakani, wakati huo huo ikiweka msisitizo kuwa viongozi wenye sifa za uongozi ndio wapewe uongozi na wao wapatapo madaraka, waelewe kuwa madaraka hayo ni dhamana ya Mwenyezi Mungu kwao, kwa hiyo watawale kwa uadilifu, bila ya upendeleo na watoe haki kwa kila mtu na sio kuwajali tu wale waliowapigia kura au waliowasaidia kupata madaraka, kwani madaraka hutolewa na Mwenyezi Mungu, hivyo misingi ya uadilifu na ya haki Aliyoiweka isipuuzwe hata kidogo na hapo ndipo amani itadumu.

Uadilifu uliagizwa hata kwa maadui pale Sheria ya Qur'an Tukufu iliposema kuwa uadui wa watu usiwahimizeni katika kuuepuka uadilifu, bali ucha Mungu unataka hata maadui wafanyiwe uadilifu na kutendewa haki. Haki inatakiwa itolewe kabla watu hawajaamua kuiomba, kwani mara nyingi watu waiombapo haki, misingi ya amani huwekwa kando na mara nyingine damu humwagika na kusababisha hali za visasi vya muda mrefu.

Islam – kama jina lenyewe lilivyo ni dini ya amani. Ni dini iliyofundisha misingi yote ya amani na ni dini inayopinga kila fundisho linaloweza kusababisha uvunjifu wa amani. Ingawaje kwa bahati mbaya baadhi ya watu wamekosea sana walipodhani kwamba Islam ni dini ya fujo na vurugu na isiyojali misingi ya kujenga amani duniani. Kwa ajili ya kuondoa uelewa huo mbaya na usio sahihi, mkutano huu ni juhudi chache katika juhudi nyingi zifanywazo na Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya duniani kote ili kuinusuru dunia dhidi ya madhara ya hatari yaliyo matokeo ya ufahamu huo mbovu. Sisi tunapenda na tunafanya juhudi ili kwamba ukweli na uzuri wa mafundisho ya dini zote ueleweke na ufuatwe na wanadamu ili sote tuweze kuishi kwa amani kama ndugu, kwani kwa asili kila dini iliyotoka kwa Mwenyezi Mungu imefundisha misingi hii ya amani.

Hata Hadhrat Khalifatul Masihi wa nne rahmahullahu alaihi, aliwahi kushauri kwamba masomo ya dini mbali mbali yenye madhumuni ya wema, ucha Mungu na maadili mema ndio yafundishwe mashuleni na kutoruhusu mafunzo ya kiitikadi tu ambayo, mara nyingine, hupindishwa na kumpeleka mtu mbali na ucha Mungu. Mafundisho ya maadili mema yanapatikana katika kila dini, basi hayo ndio yasisitizwe na kuwekwa ndani ya syllabus za masomo ya dini.

Hivyo ninawashukuru wageni wote waalikwa waliokubali kutoa muda wao kuja kushiriki pamoja nasi katika madhumuni haya yenye maana sana na ninakuombeni msikilize kwa makini yale yatakayozungumzwa ili sote tuweze kufaidika na mkutano huu.

Karibuni nyote.

Mwenyezi Mungu Ajaalie ufanisi wa nasaha hizi.

Amin.



*Amir na Mbashiri Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Tanzania Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry akimkabidhi zawadi mkuu wa Mkoa wa Pwani na Kaimu mkoa wa Dar es Salaam (wakati huo) Bibie Hajjat Mwamtumu Mahiza, ambaye pia alikuwa ni mgeni rasmi katika mkutano wa amani uliofanyika tarehe 20 April 2012 katika ukumbi wa hoteli ya Peackoc jijini Dar es Salaam*

# Hakika ya tukio la Msalaba

*Kutoka uk. 1*
watakula juu ya kichwa chake.

Huu ulikuwa ni uaguzi wa ndoto ambapo mtu yule aliota kuwa ndege wanakula mikate kichwani mwake. Ambapo uaguzi wake ni kwamba mtu huyo atasulubishwa na atakuwa chakula cha ndege. Ndege aghalabu huwa hawali kichwa cha mtu aliye hai, bali hula katika mizoga iliyoanza kuharibika kama asemavyo Yesu mwenye; "Kila penye mizoga ndipo wanapokusanyika tai" (Mathayo 24:28).

Adhabu hii pia ilitumika kama hukumu ya wahalifu wakubwa katika sheria za kidini za Waisraeli (Kumb. 21:21 - 22). Neno 'SWALABA' pia humaanisha mfupa, hasa mfuupa wa uti wa mgongo, pia ubongo wa ndani ya mfupa (Bone marrow) nao huitwa 'SULB' katika lugha ya kiarabu. Tazama kamusi za Munjid, Lane na Aqrabul Mawarid chini ya neno 'SULB'. Si hivyo tu hata katika Qur'an Tukufu mfupa huu wa mgongo umeitwa 'SULB' (Sura At-Taariq) na 'Jam'u' (Uwingi) yake ni ASWALAB (Sura 4:24) Kwa maana hii neno 'SWALABA' Humaanisha kumvunja mtu mfupa wa mgongo, tendo ambalo halina hatima yoyote isipokuwa umauti kwa aliyevunjwa.

Kwa hiyo kauli ya Qur'an Tukufu isemayo 'WAMAA QATALUUHU; WAMAA SWALABUUHU' inaweza kutafsiriwa kuwa hawakumuua wala hawakumvunja mfupa. Tafsiri ambayo yumkini inaelekea kutimiliza vyema bishara ya Zaburi inayobashiri kuwa hata mfuupa wake hautavunjwa (Zab.34:19 - 20).

Ama kuhusu hoja ya wale wanaodai kuwa Nabii Isa (as) hakupatwa na msukosuko wowote isipokuwa mtu



*Mwl. Abdallah Kh. Mbanga akiwa kwenye jukwaa akitoa hotuba katika moja ya mikutano ya Jumuiya*

mwingine aliteseka badala yake, haina msingi wowote katika maandiko matakatifu. Dhana hii haipatikani katika hadithi yoyote ya Mtume (saw) wala katika Qur'an Tukufu.

Hawa bila shaka wamefuata maoni ya Maulamaa ambao walikanganywa na neno 'WALAAKIN SHUBIHA LAHUM'lililotumika katika aya hii. Wakafasiri kuwa alifananishwa na mtu mwingine badala ya "Isipokuwa alifananishwa kwao". Aya haitaji mtu mwingine bali Nabii Isa (as) ndiye aliyefananishwa kwao. Si kwamba kuna mtu aliyefananishwa na Nabii Isa (as), bali Nabii Isa (as) ndiye aliyefananishwa. Kama tafsiri yao hii ing'ang'anizwe basi itakuwa kwamba Nabii Isa (as) ndiye aliyepewa sura ya mtu mwingine na wala si mtu mwingine kupewa sura ya Nabii Isa (as).

Katika maneno 'WAMAA QATALUUHU WAMAA SWALABUHU',(Hawakumuua wala hawakumsulubisha) kiashirio (dhamiri) cha 'Hu' kinamrejea Nabii Isa (as). Hivyo hakuna kanuni yoyote ya Lugha inayoruhusu mtu mwingine kupenyezwa ghafla katika sentensi ya mbele inayokuja mara tu baada ya hizi. Ndiyo maana hata hao wanazuoni wenye mtazamo huu wanahitilafiana juu ya nani hasa aliyefananishwa na Nabii Isa (as), kuna wanao dai kuwa Nabii Isa (as) alifananishwa na mtunza bustani, kuna wanaosema kuwa alifananishwa na mmoja wale askari waliomkamata na baadhi wanadai kuwa Nabii Isa (as) alifananishwa na mmoja wa wanafunzi wake (rejea Ruhul maani, Jalalain na Tafsir Al-Khaazin).

Kwa vyovyote viwavyo dhana hii haiwezi kuwa sawa na ndiyo maana hata waliobuni wanahitilafiana kuonyesha kuwa wana shaka na jambo hili na hawana elimu nalo isipokuwa wanafuata dhana tu.

Hivi ndivyo inavyomalizia aya hii tunayoijadili. Ni ukweli mtupu kwamba maelezo haya siyo tu hayana ushahidi wowote wa kimaandiko bali pia yanapingana hata na msingi wa Qur'an yenyewe. Kwa mujibu wa Qur'an tukufu ni kwamba kazi ya utengenezaji wa sura za watu hufanywa katika matumbo ya mama zao (3:7), kwa hivi kama ilibidi Nabii Isa (as) apewe sura ya mtu mwingine au mtu mwingine apewe sura ya Nabii Isa (as) ilibidi kwanza warudishwe katika matumbo ya mama zao ndipo wabadilishwe sura.
Hapa hoja inaweza kutolewa kwamba Allah Ambaye Yu muweza wa kila kitu, kulikoni ashindwe kumbadilisha mtu sura?

Ikumbukwe kwamba Mola wetu hufanya kazi kwa kanuni Alizojiwekea ndiyo maana Hawezi kupanga mwana, kuoa, kufa au kuumwa na kamwe hataweza kuumba Mungu Mwingine. Na katika Msingi huu huu Anatangaza kuwa kamwe hutakuta mabadiliko katika kanuni za Allah (33:63)

Waama kazi ya kubadili maumbile ya viumbe vya Mungu ni kazi ya kishetani si kazi ya kiungu, miongoni mwa ahadi za ibilisi mbele ya Mwenyezi Mungu siku aliyolaaniwa, ilikuwa ni kuwaamuru watu ili kubadili uumbaji wa Mungu (4:120), haiwezekani Mola wetu Mtukufu Naye Afanye kazi iliyomo katika ahadi za ibilisi.

Endapo mtu atasoma na kutafakari kwa makini juu ya herufi zilizotumika katika kukataa (Khurf nafii) kwenye aya hii atagundua jambo lililofichika.

Qur'an Tukufu imetumia 'MAA' badala ya 'LAA' au 'LAM', katika kukataa kuuawa na kusulubishwa kwa Nabii Isa (as) ukichunguza ndani ya Qur'an Tukufu utagundua kwamba herufi hizi aghalabu hutumika kukataa utimilifu wa jambo. Yaani halipinzi uwepo wa jambo bali hupinga ukweli wa kuwepo kwalo au utimilifu wa jambo lenyewe. Mfano mzuri ni katika aya za mwanzo za sura Al-Baqara zinazozungumzia wanafiki. Qur'an Tukufu inasema juu ya wale wanaosema kuwa tumemwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho 'WAMAA HUM BIMUUMINIIN' (yaani; na hali wao si waaminio). Ni kweli ya kwamba wanafiki si waaminio, lakini nani aliyewafahamu kuwa si waaminio? Katika hali ya kawaida wanafiki walishiriki ibada zote za Kiislam, walisali, walifunga, walihiji, walishahidia na hata kutoa mali. Lakini katika mioyo yao hawakufanya hayo kwa ikhlasi ila kwa riyaa (kujionyesha tu). Ni Mwenyezi Mungu Ndiye Aliwajua wanafiki ni kina nani. Hakuna Muislamu yeyote aliyemtambua mnafiki, hata Mtume (saw) aliwadhani kuwa ni waumini wenzie hadi pale Mwenyezi Mungu Alipomfunulia orodha ya wanafiki.

Hivyo kutumiwa kwa neno 'WA MAA HUM BIMUUMINIIN' inaonyesha kuwa ingawa walikuwa wakionekana kuwa ni waumini kwa nje lakini kwa undani hawakuwa na imani.

Tukirejeshakanunihiikatikahali ya Nabii Isa (as) kwenye tukio la msalaba kadhalika ndivyo ilivyokuwa kwamba watu wote walimwona Nabii Isa (as) kuwa ameuawa juu ya msalaba. Kwa hali ya nje alionekana kuwa ni mtu aliyesulubishwa baada ya kupoteza fahamu pale msalabani. Lakini kwa hali ya ndani Mwenyezi Mungu Alijua ya kuwa Nabii Isa (as) hakufa. Ndiyo maana Alipozinduka wafuasi wake wakaamini kuwa amefufuka toka wafu.

# Mti mzuri hujulikana kwa matunda yake

**Na Moshi Mohamedi - Nguruka, Kigoma**

**Mzee Alhaji Huseini Sabura:**
Mzee Husein Sabura alizaliwa kata ya Nguruka na Tarafa ya Nguruka Wilaya ya Kigoma mkoani Kigoma miaka themanini iliyopita. Amefariki tarehe 09/02/2012, sisi sote ni wa Mungu na kwake tutarejea.

Alhaji Mzee Husein sabura alikuwa Mzee mwenye msimamo alikuwa hayumbishwi kwa kutishwa na mtu yoyote. Alikuwa anapenda watu wa rika zote. Alichukia pale alipouziwa na alifurahi alipofurahishwa. Alipenda utani, muda fulani na alipenda kutoa methali kwa ajili ya mafundisho. Nakumbuka siku moja Mzee Sabura aliniambia methali moja kwa lugha ya Kitongwe kuwa; "Fikali Fisumbene limtitimia lisumbile nkubha" -Tafsiri viumbe vikali vinazidiana - Tetemeko linazidi radi.
Mzee Alhaji Husein Sabura alikuwa ni Muislamu wa dhehebu la Suni. Mzee huyu kwa hakika alikuwa na msimamo usiyoyumba hakujali shutuma yeyote ile toka kwa Masheikh wa dhehebu lake. Wakati nilipofukuzwa kuuza vitabu vya Jumuiyya na kufanya mahubiri katika maeneo yaliyoko mbele ya majumba ya watu, yeye aliniambia kuwa Bwana Mdogo usipate taabu na kutafuta nafasi ya kufanyia mahubiri yako, njoo hapa kwangu uuzie vitabu vyako hapa nani atakayekufuata hapa, jisikie huru na endesha shughuli zako hapa.

Kwa hakika ndipo nilipokumbuka methali ile niliyosema hapo kabla ya kwamba waliko majambazi na watoa sadaka wapo. Ushujaa mwingine aliouonyesha Mzee Husein Sabura ni huu. Siku moja kulikuwa na sherehe ya ndoa. Mdogo wake na Alhaji Sabura aitwae Juma Isela alioa siku hiyo, nami niliarifiwa katika sherehe hiyo. Kama ilivyo ada ya Wasuni, walianza kusoma milango ilipofikia mlango wa nne, watu husimama wima. Watu wote walisimama wima huku wakinengua na dufu zao. Mimi sikusimama wima, kwa sababu niliona hilo siyo tendo la Kiislamu, mimi sikuweza kusimamia ngoma. Hivyo niliendelea kukaa tu.

Baada ya tendo hilo la Qiyyamu kwisha Shehikh Sudi Athumani alimfokea sana Alhaji Huseini Sabura kwa kusema, Mzee Husein Sabura leo umetuudhi mno kutuchanganya na hawa Makadiani - makafiri, hatuwataki kabisa katika shughuli zetu, na siku nyingine mkithubutu kumkaribisha mtu huyu basi mfahamu wazi tutawasusia na chakula chenu.

Kwa hakika Mzee Husein Sabura, pamoja na ndugu yake Juma Shabani Isela hawakusema lolote walikaa kimya. Wakimsikiliza Sheikh huyo. Baada ya hapo kiliandaliwa chakula cha Bwana Harusi na marafiki zake. chakula hujulikana kama kombe la solo. Walipokaribishwa ndani Bwana Harusi na marafiki zake, Mzee Alhaji Sabura aliniita kwa kusema Bwana Mdogo Moshi twende ndani tukale chakula. Tukaingia mle ndani tukala chakula kile.
Yule Sheikh alizidi kufura kwa hasira, lakini wapi Mzee Husein Sabura hakujali lawama

*Endelea uk. 5*

# Mzee Ibrahimu Rajabu Mkoggas

## Miongoni mwa Waahamdiyya wa Mwanzoni nchini

**Na Ismail I. R. Mkoggas,**
**Dar es salaam**

Bw. Ibrahimu Rajabu Mkoggas alizaliwa mwishoni mwa vita ya kwanza ya dunia 1918 huko Rufiji katika kijiji cha Rusende/ Nyipara, wilaya ya Rufiji Mkoa wa Pwani, alikuwa mtoto wa kwanza kati ya watoto wawili wa Mzee Ibrahimu na mkewe Bi Hadija Saidi Mailo.

Katika maisha yake hakuwahi kusoma shule ingawa jesawa na utaratibu uliokuwepo wakati huo wazazi wake walimpeleka katika madrasa kujifunza kusoma Qur'an tukufu pamoja na kusomea masomo ya dini ya Islam.Mdogo wake bwana Kassim Rajabu Mkoggas ndiye aliyebahatika kupelekwa shule.

Pamoja na kwamba hakupelekwa shuleni akiwa mdogo lakini kwa jazba yake aliweza kujitafutia elimu hiyo hasa kujua kusoma na kuandika na aliweza kufanya hivyo hata kabla taifa letu halijaanzisha utaratibu wa elimu ya watu wazima. Aliwahi kuaniambia kuwa njia aliyotumia kujua kusoma na kuandika ilikuwa kuwa karibu na wanafunzi pale warudipo shuleni na kaunza kuchukua madftari yao na kuwauliza kila walichoandika. Polepole nae akajifunza kusoma na kuandika.



*Bwana Ibrahimu Kassim Mkogass akiwa anatafakari juu ya jambo fulani*

Mzee Ibrahimu aliwahi kuwa mfanyabiashara na pia mkulima. Aliwahi kufanya biashara ya kusafiri kati ya Rufiji na Tunduru. Baadhi ya wakati alikuwa akitembelea Mbeya ambako alikuweko kaka yake Mzee Omar Seif Mkoggas; hii ilikuwa ni kati ya mwaka 1940 – 1950. Mnamo mwaka 1956 alikuwa Masasi na ndipo alipopelekewa ujumbe kutoka Rusende kuwa kuna mtu anadai kuwa Masihi keshafika. Mara tu alipopata ujumbe huo aliwaambia ndugu zake msimkatae wala kumfukuza mtu huyo, tumuweke ndani mwetu, muupokee ujumbe huo na endeleeni kuishi nae, nami nakuja huko huko kwani hata nilipokuwa madrasa tulifundishwa na mwalimu wetu kuwa Masihi wa Mtume s.a.w. atakuja katika akherizamani. Mzee Ibrahimu wakati huo alikuwa nyapara wa kusimamia vibarua wa ujenzi katika Misheni ya Kikristo Masasi aliamua kuacha kazi hiyo na kurudi Rufiji kupokea ujumbe wa Masih Aliyeahidiwa, pamoja na wazazi wake na mdogo wake bwana Kassim, wote walijiunga na Jamaat Ahmadiyya. Pia ndugu wengine walijiunga na ujumbe huo. Mletaji wa ujumbe huo alikuwa ni Sheikh Salehe Mbaruku Kapilima.

Kutoka hapo mzee Ibrahimu alijitolea kuhubiri ujumbe wa Masihi kila alipokuwepo. Baadae alikwenda tena Masasi na huko aliweza kujitolea pia kufanya mahubiri na kuwafundisha watoto tafsiri ya Qur'an Tukufu na hata aliweza kufanyiwa hila na wenyeji wa huko kwa kutaka kumchinja, lakini Mwenyezi Mungu Akamnusuru.

Alinisumulia kuwa siku moja alitoka nyumbani kuelekea sokoni alipofika mahala fulani alikuta umati wa watu ukiwa umemzunguka, mara wakamuangusha chini wakamlaza huku kisu kikiwa shingoni mwake. Ghafla akatokea bwana mmoja ambaye alikuwa ni hakimu wa Mahakama; alipoona tendo lile akasema wote ninyi nawashitaki mahakamani na kuwafungeni. Kwa nini mnataka kumuua mtu kwa sababu ya imani ya dini tu? kwa vile bwana yule alikuwa ni Mkristo aliwaambia, mbona mimi nimezaliwa katika uislamu na sasa nimekuwa mkristo na mmeniacha bila ya kuniambia kama nimepotea. Aliongeza kuwaambia kwamba kwa kuanzia nitamshitaki baba yangu na nitamuweka ndani ili liwe fundisho kwa wengine. Kwa hakimu yule akafanya hivyo kwa kumfunga baba yake mzazi wiki mbili.

Baadae mzee Ibrahimu alirudi Rufiji na huko alifungua madrasa kuwafundisha watoto wa Kiahmadiyya na wengineo, miongoni mwa wanafunzi wake ni Bi Zamda Mbungiro.

Kwa wale waliowahi kumtembelea mzee Ibrahimu katika siku za ugonjwa wake watakubaliana na mimi kwamba wakati mgeni Mwanajumuiya alipomsalimia tu na kujitambulisha kwake suala la kwanza alimuuliza juu ya hali ya Khalifa Mtukufu, hali Jumuiya Makao Makuu Dar es Salaam, pamoja na hali ya Amir na wanajumuiya wengine kwa ujumla.

Hiyo inaonyesha mapenzi aliyokuwa nayo kwa Jumuiya na uongozi wake wote.

Mzee Ibrahimu alikuwa pia ni mtunzi mzuri wa Mashairi na msomaji pia.

Katika siku za mwisho wa uzee wake pamoja na kupoteza nguvu ya kuona, lakini alikuwa na kumbukumbu ya visa kadhaa vilivyowapata wakati walipoamua kujiunga na Masihi wa zama na aliendelea kuvihadithi hadi mwisho wa uhai wake. Pia aliweza kukumbuka na kuzisoma beti kadhaa za mashairi aliyoyatunga mwenyewe na yale aliyoyahifadhi kutoka kwa watunzi wengine hususan yale yaliyoimbwa kama sehemu ya malumbano na majibizano kati ya Ahmadiyya na Suni.

Mzee Ibrahim Mkogas alifariki dunia usiku wa kuamkia Ijumaa tarehe 23/ 3/2012 na kuzikwa mchana wake baada ya sala ya Ijumaa huko Mkongo, Rufiji Mkoa wa Pwani ambako ndiko alikokuwa akiishi.

Mwenyezi Mungu ampokee na kumlipa makazi yenye daraja na atuimarishe kizazi chake kubaki katika Swiraatwal Mustaqiim - Jamaat Ahmadiyya.
**Amin**.

# Mti mzuri kwa matunda yake

*Kutoka uk. 4*

za Sheikh wake. Kwa hakika asiyewashukuru watu kamwe hawezi kumshukuru Mwenyezi Mungu. Mzee Alhaji Alinisaidia mno katika mahubiri yangu hapa Nguruka. Waislamu suni walinitenda mambo mabay mno na kila mara nilikuwa nikikumbuka ile aya isemayo kwamba 'Wanataka kuzima nuru ya Mwenyezi Mungu kwa vinywa vyao, na Mwenyezi Mungu Atakamilisha nuru yake ijapokuwa makafiri wachukie' (61:9)

Wapo baadhi ya wazee wa kisuni ambao walinisaidia sana katika mahubiri yangu. Itakuwa ni dhulma kubwa kama sikuwakumbuka kwa wema wao na ujasili waliouonyesha wakati huo wa misuko suko ya mahubiri hapa Nguruka.

**Mzee Saidi Boy**

Mzee huyu Mwislamu wa madhehebu ya Sunni. Alionyesha ujasiri wake, hakuogopa lawama za Masheikh wake, ni pale aliponikaribisha katika duka lake, kwa kusema weka vitabu vyako hapa dukani nitakuuzia mimi. Kwa hakika Mzee huyu Saidi Boy Mwenyezi Mungu Atamlipa kwa wema wake.

Mtu mwingine ambaye alinisaidia mno wakati wa dhoruba lile la mahubiri ni Zonobi Elsoni. Bwana huyu Mkristo naye alinisaidia sana katika kufikisha ujumbe huu wa Masihi Aliyeahdiwa. Pamoja na Ukristo wake pamoja na kuhubiri kifo cha Yesu katika India na kulitaja kaburi la Yesu, lakini Bwana huyu alisimama imara kunisaidia hata kwa kupigana na watu wale ambao walionyesha hasira ya kutaka kunidhuru, yeye alisema, Moshi Mohamedi hapigwi na mtu yeyote hapa. Naye pia alinikaribisha dukani kwake ili niweke vitabu vyangu. Hivyo niliweka vitabu vyangu dukani kwake naye mwenyewe alikuwa anaviuza na kunikabidhi fedha zote zilizopatikana. Alhamdulillah.

**Gallos Kabogo**

Ndugu huyu naye ni Mkristo naye alinisaidia sana katika swala zima la mahubiri, huyu ndugu alinipa nafasi ya kufanyia mahubiri kwa muda mrefu. Nilifanya mahubiri katika eneo lake na vile vile aliniuzia vitabu vyangu dukani mwake. Mwenyezi Mungu Amlipe mema katika dunia na mema katika akhera.

**Mwalimu Tomma Kabogo**

Mwisho kabisa lakini si omwisho kwa umuhimu sintopenda kuacha kumshukuru Mwalimu Tomma Kabogo ambaye naye alinisaidia mno katika kazi hii ya mahubiri. Kwa ajili ya wema wake nilimpatia zawadi ya kitabu cha Reveletion, Rationality - cha Hadhrat Mirza Tahir Ahmad, Khalifatul Masih wa IV (rh) kwa jinsi alivyonisaidia katika kazi hii ya mahubiri.

Mfalme Najash wa Uhabeshi aliwasaidia Waislam wa zama za uhai wa Mtukufu Mtume (saw) pale walipofanyiwa dhulma kubwa Makka. Hivyo Mtume (saw) akawaamuru Waislamu waende Uhabeshi. Huko walipata amani. Na matokeo ya safari hiyo ya Waislamu kuindea Uhabeshi Mfalme Najashi akasilimu.

Hivyo hawa ndugu Wakristo walionisaidia katika kazi hii ya mahubiri kama si wao basi Inshallah watoto wao watajiunga na Jumuiyya hii.

# Bustani ya Washairi

## UFIKO

1. Utu wataka ufiko, wa kutambua miiko,
Uletao mnyooko, mtu apate mashiko.

2. Nalia wengi tuliko, tungali na mtindiko,
Mawazoni mchafuko, hatujui tuendako.

3. Tukokwenyemcharuko,kwenyemwongozohatuko,
Hatujaketi kitako, kitako cha fikiriko.

4. Tumejitia kwaziko, kwa yetu mikengeuko,
Hatujali maanguko, tumefumbwa mfumbiko.

5. Mola Utupe mwamko, tusikie tuitwako,
Roho zipate geuko, tuelekee Uliko.

6. Tuangazie ufiko, tufikie yakiniko,
Tuepushie mafiko, yaletayo fadhaiko.

7. Jalia mwisho tuweko, Radhi Allahu waliko,
Walioshika mwitiko, wakapata sameheko.

**Musa Mpinga**
**Dar es Salaam**

## KUJA KWA MASIHI WETU

1 Sifa ni za Mola wetu, Muumbaji na Mlezi
Aliyetuumba watu, akaweka viongozi
Naye mbora wa watu, ni Muhammad mpenzi
Twakushukuru Mwenyezi, kuja kwa Masihi wetu

2 Kuja kwa Masihi wetu, twakushukuru Mwenyezi
Yeye ni mbora wetu, kazikwea hizo ngazi
Bali ni wajibu wetu, kumtii kiongozi
Twakushukuru Mwenyezi, kuja kwa Masihi wetu

3 Akhsante Mola wetu, ulofanya maamuzi
Kazaliwa kati yetu, Nabii wa zama hizi
Wema, huruma na utu, ukampa ya Azizi
Twakushukuru Mwenyezi, kuja kwa Masihi wetu

4 Amedhihirika kwetu, kaja ni wetu mlezi
Qur'an sheria yetu, yeye akawa mlinzi
Umma Muhammad wetu, yeye ndiye mtetezi
Twakushukuru Mwenyezi, kuja kwa Masihi wetu

5 Islamu dini yetu, imeng'aa mbalamwezi
Msubiriwa wa watu, kuja kuzitenda kazi
Ahmad amefutu, barazani pa Mwenyezi
Twakushukuru Mwenyezi, kuja kwa Masihi wetu

6 Katutatulia watu, yeye ndiye mtatuzi
Njia ya kwa Mola wetu, akawa muelekezi
Huyu ndiye nuru yetu, tuondolewe simanzi
Twakushukuru Mwenyezi, kuja kwa Masihi wetu

7 Ahmadi nuru yetu, tuondolewe simanzi
Elimu ya dini yetu, katuongeza ujuzi
Alivyotufunza watu, tazama yetu malezi
Twakushukuru Mwenyezi kuja kwa Masihi wetu

8 Kafufua dini yetu, hiyo ndiyo bora kazi
Kakuza heshima yetu, milango ikawa wazi
Ukhalifa kito chetu, nyuma yake fatilizi
Twakushukuru Mwenyezi, kuja kwa Masihi wetu

9 Hiyo ni thamani yetu, Ahmadiyya pongezi
Hisani ya Mola wetu, tumepewa viongozi
Msada wa dini yetu, rahisi kutenda kazi
Twakushukuru Mwenyezi, kuja kwa Masihi wetu

10 Wampingao wenzetu, hivi hawajiulizi
Hisani ya Mola wetu, Amefanya uteuzi
Waache ubishi watu, wafanye upelelezi
Twakushukuru Mwenyezi, kuja kwa Masihi wetu

11 E,Mwabudiwa wa watu, twaomba wako ulinzi
Katika hii swiratu, uwe wetu muongozi
Adui asithubutu, asilete uchochezi
Twakushukuru Mwenyezi, kuja kwa Masihi wetu

**Mwl. Mubaraka A. Nyamihasi**
**S.L.P 391 - Tarime, Mara**

## UKHALIFA KWETU NEEMA

1. Kuukana ni msiba, ukhalifa kwetu neema,
Neema ilo matwilaba, gizani ndiyo najima,
Najima tena ni twiba, pulikeni enyi umma,
Ukhalifa kwetu neema, kuukana si twayyiba.

2. Kuikana si twayyiba, zawadi yake Karima,
Zawadi 'letayo hiba, hiba kwa wetu Rahima,
Iletayo ukuruba, habithi akawa mwema,
Ukhalifa kwetu neema, yatutenga na ghadhaba

3. Yatulinda na ghadhaba, ilowapata wa nyuma,
Walojitia ujuba, kuwakana Maasuma,
Salehe na Shuwaiba, Issa, Musa na Adama
Ukhalifa kwetu neema, ndimo ulimo uzima.

4. Binadamu huwa fisi, ama ageuke kima,
Tena huwa mufilisi, akaondokwa hekima,
Akamba ana mkosi, akosapo hii neema,
Ukhalifa kwetu neema, ndimo ulimo uzima.

5. Yatuondoa yabisi, ikang'arisha mitima,
Ukaisha wasiwasi, wa kwenda kwenye hutwama,
Makao yao waasi, nari yenye kurindima,
Ukhalifa kwetu neema, hidaya yake Quddusi.

6. Sisi tutakuwa sisi, neema tukiiandama,
Tutang'ara ja fususi, daima dumu dawama,
Naima firdausi, 'takuwa yetu makama,
Ukhalifa kwetu neema, amabate ewe insi,

7. Acheni ukaramsi, ushupavu siyo mwema,
Ni kundi la Ibilisi, lisilo na mwisho mwema,
Huyahandisi maasi, kuwaudhi walo wema,
Ukhalifa kweu neema, chonde chonde msiasi.

8. Hawanayo kumbukumbu, mashehe wasio soma
Huonyesha umbumbumbu, wakanapo hii neema,
Ndiyo wachujao m'mbu, ndovu akapita wima,
Ukhalifa kwetu neema, ndiyo wetu utibabu.

9. Sasa nichimbuwe chimbu, mjue msio soma,
Namanga hadi Nanyumbu, sikiza ninayo sema,
Msifuate mkumbu, fanya mambo kwa kupima
Ukhalifa kwetu neema, chasema chema kitabu.

10. Twasoma kwenye kitabu, kilichajaa hikima,
Tanzilu yake Wahabu, swiratwa muustaqima,
Sura 'nuru' yahutubu, kwendelea kwa naima,
Ukhalifa kwetu neema, ni kitaba Maktubu.

11. Kunjua ukiratibu, Qadifulaha kisoma,
Juzuu kwenye kitabu, Qara' ya saba tizama,
Aya imestahabu, ahadi yake Hakima,
Ukhalifa kwetu neema, tangazeni wahutubu.

12. Nazidi wapa sahifu, msome mnaosoma,
Asaa mkasadifu, uwaishe uyatima,
Wa kukosa Ashirafu, kiongozi alo mwema,
Ukhalifa kwetu neema, habili yake Raufu.

**Mwalimu Majid A. Sudi, (Simba Dume)**

## AWE KHAIRUN NISAA

1. Ewe Muumba dunia, na vyake vilivyo jaa
Makini unavilea, visipate kusinyaa
Kheri ulotujalia, iwe kheri ya kufaa
Awe Khairunnisaa, Mola takabali dua.

2. Mola takabali dua, awe Khairunnisaa
Tuwezeshe kumlea, akae na kutambaa
Makuzi yenye mbolea, yasisitishwe na njaa
Awe Khairunnisaa, Mola takabali dua.

3. Mhifadhi kuugua, asije akadumaa
Muwahishe kutembea, asipate kuzubaa
Mfunze na kuongea, semi zisizo mawaa
Awe Khairunnisaa, Mola takabali dua.

4. Qur'an nalilia, awe na chema qiraa
Fahamu za kusomea, shuleni awe ang'aa
Ajue kuvumilia, asiyekata tamaa
Awe Khairunnisaa, Mola takabali dua.

5. Mjalie kufikia, ngazi za kiulamaa
Kwenye fani kubobea, mpe na hii sanaa
Kwa ajiliyo Jalia, apambane kishujaa
Awe Khairunnisaa, Mola takabali dua.

6. Kwenye yako Jumuia, kwa wenzake awe taa
Ajuaye shauria, yaletayo manufaa
Asikose hudhuria, Shura na Ijtimaa
Awe Khairunnisaa, Mola takabali dua.

7. Mfanye mwenye khushua, mthamini Ijumaa
Apendaye sujudia, na kurefusha rakaa
Asiyechoka kutoa, mtimiliza zakaa
Awe Khairunnisaa, Mola takabali dua.

8. Umpe njema tabia, mwenye kujali kuvaa
Mweledi kuchunga njia, mwerevu penye hadaa
Upuuzi kuchukia, mpiga vita zinaa
Awe Khairunnisaa, Mola takabali dua.

9. Mambo yasiyo sawia, kwake yawe ni kinyaa
Umpe kali hisia, za wengine kushangaa
Pindi wakimuitia, ya kwao kuyakataa
Awe Khairunnisaa, Mola takabali dua.

10. Awe fundi wa kulea, mhifadhi ujamaa
Mwingi wa kusubiria, mpole penye fadhaa
Bingwa wa kudhukuria, mtegemea samaa
Awe Khairunnisaa, Mola takabali dua.

11. Apende kutumikia, wote waliomzaa
Pia kuwashukuria, walomzidi masaa
Fani za kusaidia, aponye hadi vichaa
Awe Khairunnisaa, Mola takabali dua.

12. Mwisho ninamuombea, Umrefushe wasaa
Mola Ukipendelea, ende makumi tisaa
Hayo yakishatimia, umruzuku kupaa.
Awe Khairunnisaa, Mola takabali dua.

***Abdulrahman M. Ame, Dar es Salaam***

## KARIBU WETU MGENI

1 Kwa jina la Rahmani, Ya Rabbi Mola Mkwasi
Twakushukuru Manani, Kutuletea nemsi
Ni benati Khairun, kaja jiunga na sisi
Karibu wetu mgeni, uje jiunga na sisi

2 Mpe tunda la yakini, Akuabudu Qudusi
Jingine asitamani, baya na lenye nuhusi
Asiguse asilani, tunda lake ibilisi
Karibu wetu mgeni, uje jiunga na sisi

3 Mpe mapenzi ya ndani, kupenda wetu Raisi
Khatama wa Nabiyini, Kiongozi wetu sisi
Ni Muhammadi Amini, ampe kubwa nafasi
Karibu wetu mgeni, uje jiunga na sisi

4 Elimu ya Qur'ani, ya ndani yenye fususi
Mpatie kwa undani, vipande vya alimasi
Akae nayo mwilini, mithili kama libasi
Karibu wetu mgeni, uje jiunga na sisi

5 Mzawa wa Qadian, chimbuko lake Farisi
Alokuja hami dini, na kuleta ufanisi
Akubali yake shani, pasipo na wasiwasi
Karibu wetu mgeni, uje jiunga na sisi

6 Nidhamu yetu makini, ing'arayo ja shamsi
Ukhalifa wa thamani, kwa faida ya unasi
Binti awemo kundini, akihami taasisi
Karibu wetu mgeni, uje jiunga na sisi

7 Kaditama kituoni, Ham sina wasiwasi
Ninayo kubwa imani, Utampa ikhilasi
Ili aje tuauni, tuwe mbali na maasi
Karibu wetu mgeni, uje jiunga na sisi

***Mahmood Hamsin Mubiru***
***(Wa Mamba) Dar es Salaam***

# Kifo cha Mwalimu Majid Sudi kimenifanya niyapende mashairi

**Mhariri Mapenzi ya Mungu;**

Mimi sikuwa mpenzi kabisa wa mashairi. Sijawahi kusoma au kusikiliza redioni hata kipindi kile cha ukiritimba wa vyombo vya habari nchini ambapo mashairi yalikuwa yanachapishwa na magazeti ya serikali na kusomwa na redio ya Taifa (RTD). Nikiri kutoka moyoni kuwa hata kwenye mikutano yetu kule Kitonga au kwingineko wakati wa usomaji shairi ndio wakati wa kuhamisha mawazo (CONCENTRATION) yangu kutoka kwenye mkutano na kuyapeleka sehemu nyingine au hata kwenda kupata madafu (Kitonga) au kingine chochote. Lakini kifo cha Mwl. Majid Sudi Namwete kimenifanya niyageukie mashairi na hasa baada ya kusoma makala ya Mapenzi ya Mungu toleo No. 68 la Januari 2012 lenye kichwa "MATUMIZI MEMA YA KIPAJI" na Wamamba. Makala hiyo ilinivuta niyasome mashairi ya toleo hilo. Nilisoma kwa mazingatio makubwa beti za "Simba katutoka" za Mwl. Mbanga na nikagundua kweli mashairi yana ujumbe mzito ambao hutolewa kwa njia ya mkato.

Mashairi yaliyoelezea kifo cha Mwl. Majidi ya Mwl. Mbanga, Mwl. Mbaraka A. Nyamihasi wa Tarime na Mwl. Najat Fakim Said wa Mafisa Kilindi Tanga yalinifanya nitiririkwe na machozi, ingawa siku ya msiba, pamoja na ishara kubwa ya safari ya Mwl. Majid ya wingi wa waombolezaji haikunifanya nitoe machozi.

Ombi langu kwako mhariri kama kuna uwezekano utoe walau mashairi ya marehemu Mwl. Majid Sudi kidogo kidogo kwa kadri nafasi itakavyopatikana ili tufaidi (nifaidi?) hekima zake kwani, ni kawaida ya binadamu, mtu anapofariki ndipo mambo yake au hekima zake watu huzifuata na kufanya marejeo. Ndipo utakuta wanamuziki wanapokufa kanda zao (santuri) zinapanda kwa mauzo, na wengine kujaribu kuwafanya marehemu zao "wenye heri" baada ya miaka kibao ya vifo vyao.

**Said C. Masud (Afande Said)**
**Wa Polisi Traffic Dar es Salaam.**

**Katika toleo hili tumeanza kuweka moja ya shairi la Mwalimu Majid Sudi kuhusu Ukhalifa na Inshallah tutaendelea kufanya hivyo sawa na ombi la msomaji wetu.**
**Mhariri**



*Mwalimu Majid Sudi enzi za uhai wake kitoa hotuba katika moja ya mikutano ya Jumuiya*

# Maswali ya Mkristo yajibiwa

**Na Mwalimu Kais Ally - Mkongotema, Songea**

Ewe ndugu yangu mpendwa, Assalaam Alaikum. Napenda kuchukua fursa hii kujibu maswali yako ambayo umenitaka niyajibu kwa njia hii ya kuandika.

**Swali la kwanza (I):** Umeuliza kuwa; "Je Yesu unamtambuaje?"
**Jibu:** Yesu ni Mtume wa Mungu. Na maneno ya Yesu mwenyewe yanathibitisha hivyo: "Akajibu akasema sikutumwa ila kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli Mathayo 15:24, Yohana 17:3 pia Yohana 8:42.

Mimi siwezi kufanya neno mwenyewe; kama nisikiavyo ndivyo nihukumuvyo na hukumu yangu ni haki, kwa sababu siyatafuti mapenzi yangu mimi, bali mapenzi yake aliyenipeleka Yohana 5:30 - 6:38 - 4:36.

**Swali la pili (A):** Kwa nini Yesu asiwe Mungu?
**Jibu:** Yesu si Mungu kwa sababu hakuna andiko lolote ndani ya Biblia linalosema, Mwenyezi Mungu amesema kwamba Yesu tumwite Mungu, na pia hakuna aya yoyote ndani ya Injili ambayo bwana Yesu amedai kuwa yeye ni Mungu kama ipo tafadhali nionyeshe.

**Swali la pili (B):** Umenitaka nisome Yuda 1:25 ambayo ina maneno yafuatayo; "Yeye aliye Mungu pekee, Mwokozi wetu kwa Yesu Krsito bwana wetu, na ukuu, na uwezo, na nguvu tangu milele, na sasa na hata milele. Amin"
**Jibu:** Kifungu hicho kinaonesha wazi kuwa siyo madai ya Yesu wala si tangazo la Mungu bali inaonekana ni mapenzi ya mwandishi mwenye shauku ya kuokolewa na Yesu. Ninalohitaji ni ushahdi wa yeye mwenyewe Yesu aliposema 'mimi ni Mungu'.

**Swali la pili (C):** Hii ina maana gani; Mungu Baba, Mungu Mwana, na Mungu Roho Mtakatifu?
**Jibu:** Maneno yako haya tungepata ufafanuzi toka kwako. Waila sisi Waislam hatuamini katu kuwa Mwenyezi Mungu amegawanyika vipande vipande bali hata vifungu chungu mzima ndani ya Biblia vinatuunga mkono kuwa MUNGU NI MMOJA TU. Mathalani 2 Wafalme 19:15, Zaburi86:10, Yohana 17:3,, Yohana 5:44, 1Wakorintho 8:4 - 6, Marko 2:7 n.k.

**Swali la pili (D):** Yohana 1:1 - 34 ina maana gani?
**Jibu:** Kifungu hicho ulichotakiwa ni kunifahamisha kuwa kina maana gani siyo mimi nitowe maana. Na kwa kuwa wewe umeshindwa kukielewa na kwa kweli kifungu hicho hakieleweki hata kwa mwalimu wa chuo kikuu. Mathalani inasemwa: hapo mwanzo kulikuwa na kiti, nacho kiti kilikuwa kwa Seremala, nacho kiti kilikuwa Seremala. Je wewe umeelewa nini?

**Swali la pili (E):** Yohana 3:16 ina maana gani?
Kifungu hicho kinasema: "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa mwanae wa pekee ili kila mtu amwaminiye asipotee bali awe na uzima wa milele"
**Jibu:** Kwa hakika Injili imetumia neno "mwana wa Mungu" kwa ajili ya mtu mwema, na watu wabaya wameitwa wana wa shetani. Hata Mayahudi ambao walibishana na Yesu walisema "Baba yetu ni mmoja Mungu" YH 8:41. Yesu aliwajibu akasema, ninyi mmetoka kwa baba yenu shetani (Yohana 8:44) kwa sababu walimkadhibisha Nabii wa Mungu.

**Swali la tatu:** Mbona ninyi muonapo mwezi mnafunga na kuabudu kwani mwezi ndiyo Mungu?
**Jibu:** Ndugu yangu mpendwa ufahamu wazi kuwa Waislamu hawaabudu mwezi bali hawaabudu chochote isipokuwa tunmwabudu Mungu mmoja tu tena asiye na mshirika. Bali kufunga saumu mwezi wa Ramadhani ni Amri iliyotolewa na Mungu ambayo inatakiwa kutekelezwa mara tu baada ya kuuona mwandamo wa Mwezi na amri hiyo itaishia baada ya kuandama mwezi mwingine kama ilivyo kwa Wakristo ibada hii ya kufunga inapatikana ndani ya mwezi wanaouita Kwaresma.

**Swali la nne:** Yuda ISKARIOTE ndiye Mwenye kumsaliti Yesu, je munaamini kuwa Yesu alisalitiwa?
**Jibu:** Ukisoma Mathayo 27:3-8 neno "Kusaliti" linapatikana hapo na kila mwenye kusoma andiko hilo ataamini hivyo. Hata mimi naamini hivyo ingawa nashangazwa kuona bwana huyo Wakristo hawampi heshima ya kuwa naye ni mkombozi namba mbili kwani bila yeye Yesu alishajificha na asingekamatwa na kuwambwa msalabani kunakosemwa na Wakristo kuwa chanzo cha ukombozi. Kinyume chake Jamaa huyo amelaaniwa hata akafa kwa ajali mbaya ya kukatika vipande vipande.

**Swali la tano:** Mbona mnapenda sana Biblia kuliko Qur'an tukitaka kujifunza Qur'an tutaelewa vipi, naona hakuna haja ya Qur'an?
**Jibu:** Sisi hatupendi sana Biblia bali tunapenda sana Qur'an Tukufu. Tungependa Biblia ungetuona makanisani tukiimba na kupiga vinanda n.k, waila tunatumia vifungu vya Biblia si kwa maana ya kuipenda bali tunaonyesha kwa urahisi udhaifu wa mafundisho ya Kikristo. Nawe ukitaka kujifunza Qur'an ipo bayana tu kwani inasomeka katika Kiswahili.

**Swali la sita:** Mbona Yesu munamuamini sana lakini hamuamini kuwa ni mwana wa Mungu? Yohana 3:16.
**Jibu:** Islamu inamwamini Yesu kuwa ni Nabii wa Mungu tu tena kwa wana Waisraeli tu. Mathayo 15:24. Yesu si mwana halisi wa Mungu bali Yesu ni mwana wa binadamu sawa na maandiko. Basi mwana wa binadamu hawezi kuwa Mungu wala mwana wa Mungu Mathayo 11:19, Mathayo 12:40. Kama Yesu ni mwana wa Mungu wa kuzaliwa na Mungu basi ndani ya Biblia mwana si Yesu peke yake. Mfano "Israeli mzaliwa wa kwanza wa Mungu - kutoka 4:22, Daudi mwana wa kwanza wa Mungu Zaburi 89:26 - 27, Yohana 10:34.

**Swali la saba:** Naomba maana ya Israeli na Waisraeli Mathayo 2:43 maana ya uwingi na umoja? Mohamad mbona sijasikia sifa katika Biblia?
**Jibu:** Israeli ni Yakobo na Waisraeli ni kizazi cha Yakobo soma kitabu cha Mwanzo. Mathayo 2:43 hakipatikani katika Biblia. Bishara au sifa za Mohamad soma vifungu vifuatavyo: Kumb.18:18 - 19. Mtume mfano wa Musa atakuja. Nabii yule hajaja matendo 3:18 - 22 ufalme wa Mungu watapewa watu wengine Mathayo 21:43.

Bishara ya tano - Yesu uzao wa Israeli na Waisraeli Mathayo 21:43 = utabiri unasema: Ufalme wa Mungu utaondolewa kwenu nao watapewa Taifa lingine ..... (Yaani Taifa lingine ambalo si Waisraeli. Yesu ni Mwisraeli utabiri huo haumhusu. Bali utabiri huo umetimia kwa kuja Nabii Muhammad (saw) kwenye Taifa la Waarabu.

**NB: Maswali haya yameulizwa na muumini wa Kanisa la Romani Katoliki (Madaba Songea) ambaye hakutaka jina lake litajwe kwenye gazeti.**

# "Mwelewe Maulvi Nuruddin"

# Hadhrat Khalifatul Masih I r.a.

*Hiki ni kitabu kilichoandikwa na Sir Muhammad Zafrullah Khan r.a. na kutafsiriwa kwa Kiswahili na Sheikh Jamil Rahman Rafiq*

**Kutoka toleo lililopita**

**MAWAIDHA YA MWISHO**

Dkt. Bhagwan Das Kushta, Mwalimu Mkuu wa shule moja katika Saharanpur, alihudhuria mbele ya Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. tarehe 22 Machi 1913, na akatangaza kukubali Islam. Akamsihi Mwislamu mpya huyo akisema:

"Hakuna apasaye kuabudiwa isipokuwa Mungu pekee Aumbaye na kumjaalia mtu mahitaji yake yote. Hakuna yeyote mwingine anayestahiki kuabudiwa wala kuchukuliwa kuwa Mungu. Kumwabudu yeyote minghairi yake ama kumsujudia ni ushirikina. Pamoja na kuagiza kuamini Umoja wa Mungu, Islam inataka pia kumwamini Muhammad s.a.w. kuwa mtumishi Wake na Mjumbe Wake. Kwani, katika zama zilizopita alipodhihiri duniani wakati wowote mtu mwema, wafuasi wake, baada ya muda fulani, wakamfanya mungu. Hiyo ndiyo ilitendeka kumhusu Ram Chandra a.s. na Krishan a.s. Yesu a.s. pia akafanywa Mungu, akaitwa Mwana wa Mungu, ingawaje alisema: Mbona waniita mwema? Hakuna mwema isipokuwa Mungu. Kwa hiyo, Mtume Mtukufu s.a.w. akaogopa isije yeye naye akafanywa mungu akaongeza katika shahada: 'Hakuna mwabudiwa ila Mungu,' na kwamba yeye yu mtumishi na Mjumbe wa Mungu.

Jiha ya pili ya Islam ni huruma kwa viumbe wa Mungu. Zaka na Hija hutilia moyoni huruma ya watu, na sala na saumu humfanya mtu kujihurumia, kuna baraka kubwa katika saumu. Hiyo humzoesha mtu kuepukana na matumizi yasiyo halali ya kitu chochote; kwani yule anayejitenga mbali na kile kilicho halali katika saumu, lazima atatenganana kilichoharamishwa na Muhammad s.a.w. kama akimwamini yeye. Basi maana ya kanuni ya imani ndiyo kusisitiza Umoja wa Mungu na kwamba Muhammad s.a.w. ni mtumishi Wake na Mjumbe Wake, na kwamba sala, saumu, Haji na zaka vimewekwa kwa faida ya mtu binafsi na pia kwa jamii nzima. Kuna faida gani kumnyunyuzia mtu maji kama alama ya kukubali imani? Yesu alisema, ni rahisi ngamia kupita ndani ya kitundu cha sindano kuliko tajiri kuingia katika ufalme wa Mungu."

Katika kharifu (msimu baina ya kiangazi na kipupwe) na kipupwe cha mwaka 1912-1913, Sahibzada Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad r.a. alikwenda kutembelea Misri na Hijaz na katika safari hiyo akahiji pia. Akarejea Qadian Februari 3, 1913. Mnamo kiangazi cha mwaka huo akaamua, kwa kupata kibali cha Hadhrat Khalifatul Masihi r.a., kuanzisha kutoa gazeti la kila wiki ambalo Hadhrat Khalifatul Masihi akaliita *Al-Fadhl*. Tolea la kwanza lilitolewa Juni 19, 1913. Baadaye likawa gazeti la kila siku na sasa tangu zaidi ya nusu karne ni gazeti la Jumuiya ya Ahmadiyya.

Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. akashikwa na homa kali sana mnamo Juni 25. Keshoye, ijapokuwa alikuwa bado dhaifu, akatoa darasa la Qur'an Tukufu, na mwishowe akanena:

"Niuguapo, nachelea kwamba pengine ndio mwisho, safari hii pia nikafikiri hivyo. Nikasali *Rakaa* mbili. Katika *Rakaa* ya kwanza baada ya sura *Fatiha* nikasoma sura *Dhuha* (93) na katika *Rakaa* ya pili Sura *Inshirah* (94). Kisha nikashughulikia kumsifu Mungu na kuomba ghofira. Ndipo nikaomba dua ambayo nina yakini imepokelewa. Narudia ili nyote mshirikiane katika hii. Nayo ndiyo hii: Hakuna apasaye kuabudiwa isipokuwa Mungu, Mjuzi wa kila kitu, Mpaji. Hamna mwabudiwa minghairi ya Mungu, Mola wa Arshi kuu. Hamna mwabudiwa ila Mungu, Mola wa mbingu na ardhi, Mola wa Arshi Tukufu. Nakuomba njia za kuvutia rehema Yako, na njia imara za kupata msamaha Wako, na hadhi kubwa ya kila wema, na usalama katika kila dhambi. Usiache kosa langu lolote bila kulisamehe, wala ghamu yangu yoyote bila kuiondoa, wala mahitaji yangu yoyote ya kweli bila kuyatimiza, Ewe Uliye Mrehemevu sana. Mola, tumeelemewa sana kutoka kila upande, Islam imeshambuliwa vikali. Waislamu ni walegevu, wana elimu haba ya dini, au ya Qur'an Tukufu, au ya mfano wa Mtume Mtukufu s.a.w. Maadui wanasonga mbele. Mola, mwinue mtu mwenye kuvutia, asiye mzembe, shujaa sana, mvumilivu, mwenye kukimbilia daima kuomba dua, mwenye kutimiza matakwa yako, mtaalamu wa ujuzi wa Qur'an Tukufu na Hadithi za kweli. Tena Umjaalie Jumuiya ambayo wanajumuiya wake wawe na sifa hizo zote. Mola, kama kuna majaribio, basi wajaalie imara, na Usiwatwishe mizigo wasiyoweza kuibeba (2:287); na Uwakuze jinsi nilivyoomba.

Nahisi Mungu Atatimiza utashi wangu. Nyinyi nanyi mwombe kwa moyo huo, na muwe wasaidizi katika njia ya Mungu."

Keshoye ilikuwa Ijumaa, akawasihi jamii ya waabuduo katika hotuba ya pili kama ifuatavyo:

"Sina la kukazania isipokuwa maombi. Dumuni kufanya maombi. Nawasisitizieni hiyo kwa manufaa yenu. Sitaki kutoka kwenu chochote, hata kwamba mwinuke kwa kuniheshimu. Kama ningalitazamia chochote kwenu, ningalifanya kosa kubwa kabisa la utovu wa shukurani kwa Mungu. Je, Yule Mungu Aliyenijaalia fadhili zake sikuzote, zaidi kuliko nilivyotazamia, Atanifanya sasa niwategemeeni katika uzee wangu kwa siku zangu chache zilizobakia?

…. Fadhili zake zifululizazo zanilazimisha niwe Wake kikamilifu. Nguvu zangu zote ni fadhili Zake, heshima zote na taadhima nilizo nazo ni zawadi Zake."



*Maulana Hadhrat Hakeem Nuruddin Khalifatul Masih I r.a.*

Ni la kushangaza kwamba mawaidha yote ya Hadhrat Khalifatul Masihi r.a ya kusisitiza mwafaka na umoja baina ya wanajumuiya, maonyo yake yote kuhusu matokeo ya kuogofya ya mafarakano na fitina, yakawaathiri wafitini wagumu kwa kitambo kidogo tu, kama yaliathiri kwa vyoyote. Kwa hakika wakaonekana kukaza ukaidi wao. Ni kweli ya kwamba jumuiya kwa jumla kwa kutahadharishwa ipasavyo na kuonywa ikasalimika katika ujanja mbaya wa watu wachache wenye mikono mirefu wasiotaka kupatana; na huo kweli ulikuwa ufaulu mkubwa. Hata hivyo ni jambo la kujutia kwamba mtengano haukuweza kuepukika.

Uongozi wa wafitini ulikuwa na nguvu katika Lahore. Afya ya Khalifatul Masihi r.a. ilipoendelea kwa vyovyote kuwa hafifu na ikaanza kuharibika, kundi la wafitini likaanza kufanya propaganda kwa ushupavu kukabili hatari isiyoepukika. Hatua ya kwanza waliyochukua ni kwamba wakaanza kutoa gazeti kutoka Lahore waliloita *Paighame Sulh* (Ujumbe wa Amani). Toleo la kwanza lilitolewa Julai 10, 1913. Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. akawa mnunuzi wake, lakini baadaye akakataa kulipokea, kwa kuona madhara ya sera zake na kazi yake hata kwamba akaliita *Paighame Jang* (Ujumbe wa Vita). Mara kwa mara ahadi za uaminifu kwa Khalifatul Masihi r.a. zilichapishwa, lakini walipungukiwa nia. Ilipigwa kampeni mfululizo kumvunjia heshima Shaibzada Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad r.a. Walichelea isije Sahibzada Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad, japo alikuwa kijana tu, akachaguliwa kuwa *Khalifa* baada ya Khalifatul Masihi r.a. ambaye hakuficha kwamba alimheshimu sana Sahibzada. Itikadi na mafundisho ya Jumuiya ya kupambanua yaliyotolewa na Masihi Aliyeahidiwa a.s. yalielezwa mara kwa mara na Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. na hadi wakati huo yalikuwa yanakubaliwa na viongozi wa wafitini wenyewe, yakaanza kubomolewa taratibu na kuzimuliwa na wafitini kwa nia ya kupendwa na Waislamu wengi wasiokuwa Waahmadiyya.

Ijapokuwa afya yake iliendelea kuharibika Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. alitoa darasa la Qur'an Tukufu nzima katika mwezi wa Ramadhani mnamo Agosti – Septeba 1913.

Shambulio kubwa zaidi lilifanywa kwa niaba ya wafitini kutoka nyuma ya pazia nyembamba na ya woga katika Oktoba 1913, kwa sura ya vijitabu vidogo viwili bila ya jina la mwandishi, kimoja baada ya kingine katika kitambo kifupi, vilivyoitwa *Idh-harul Haq I* na *Idh-harul Haq II* (kudhihirisha haki). Vilikuwa vichafu na vya aibu, vilivyojaa madai ya uwongo ya uchongelezi dhidi ya Hadhrat Khalifatul Masihi na watu wa familia ya Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa a.s., akiwemo Hadhrat Ummul Muminin r.a. pia. Kweli hii kwamba vilitolewa hivyo kwa kushauriwa na viongozi wa wafitini – ingawa walikana – inahakikishwa na maneno ya Mahriri wa *Paighame Sulha* la 16 Novemba 1913, ambayo ni haya:

"Tumeona katika vijitabu hivyo kwamba maneno mengi yaliyoandikwa humo hayana shaka hata kidogo kwamba ni ya kweli.... Kama *Ansarullah* ya Lahore ikiona inafaa kujiingiza katika habari hii na kukusudia kuandika chochote dhidi yetu ili kuzalisha kuelewana kubaya kwa sababu tumeyaunga mkono maneno yaliyomo ndani ya vijitabu hivyo, hapo lawama itakuwa juu yao kama tukichapisha lolote kwa kujibu."

Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. akaiagiza *Anjuman Ansarullah* kutayarisha na kuchapisha majibu ya vijitabu hivyo. Muswada wa majibu ulipopelekwa kwake, akaukagua na akandika juu yake: *Paigham (Sulha)* linastahili kupata lawama elfu kwa kutuletea ujumbe wa vita kwa kuchapisha barua yake wazi, na kwa njia hiyo limetangaza unafiki wake. Amelaaniwa yule anayezindua msiba ulalao.

Majibu yalitolewa katika vijitabu viwili: *Khilafat Ahmadiyya* kikachapishwa Novemba 23, na *Idh-ahare Hakikat* tarehe 28 Novemba 1913. Majibu hayo yakathibitika kuwa yenye kuathiri mno kama kanusho kamili la masingizio na uchochezi ya kuadhiri na ya uwongo yaliyoandikwa katika vijitabu vya kuchukiza, na yakailinda Jumuiya kikamilifu dhidi ya fitina ambayo vijitabu vyao vilikusudia kuchochea.

Khalifatul Masihi r.a. alipougua sana baada ya kuanguka kutoka juu ya farasi jike, akaona katika ruya kwamba mtu fulani ametia rupia moja mfukoni mwake. Akaagua kwamba atapata mwana. Ruya hiyo ikatimia tarehe 18 Novemba 1913 ambapo alijaaliwa mwana wa tano aliyemwita Abdullah.

Mkutano wa Mwaka wa 1913 ulifanyika Desemba 25-27. Wahudhuriao walikuwa wengi zaidi kuliko mwaka uliopita. Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. akiendelea kuhutubia alinena:

"Kutimiza mapatano ni jambo la faradhi. Nawaelekezeni kwenye ahadi mojawapo ili muweze kutafakarikwambamnaitekeleza. Ndiyo ahadi ya utii mliyofanya nami. Tena kati yenu kuna wenye hali mbaya wasemao: *Khalifa*, ati, ni nini? Yu mkongwe. Angalieni, sikilizeni na kumbukeni ya kwamba Mungu Mtukufu Amenifanya *Khalifa*, nami simtegemei yeyote kati yenu kwa chochote. Nimekwisha omba dua kulindwa na matokeo ya uzee, na Yeye Amenihifadhi. Amenijaalia ujuzi wa Neno lake. Kunilaumu kwenu hakukubaliwi na Mungu. Yeye Ana ghera kwangu. Tubuni kwa fikira yenu mbovu. Yeye Amehifadhi kikamilifu nguvu zangu. Sifa zote njema ni Zake kwa fadhili Zake zote.

Nyinyi hamna uhuru wa kueneza habari zinazohusikana na ulinzi au hatari. Mwapaswa kumfikishia chochote cha aina hiyo Amiri au Mwenyekiti wenu ili aweze kuchukua hatua yoyote ifaayo. Waliochapisha vijitabu viwili, *Idh-harul Haq*, na barua moja ya wazi kwa *Ansarullahi*, na kuendeleza majadiliano juu ya *Ukhalifa*, hawakuwa na madaraka kufanya hivyo. Barua ya wazi iliniudhi sana moyo wangu. Tena mtu fulani akaniletea kadi iliyochapishwa na akaniomba ruhusa kuichapisha. Nikamwambia hiyo ni kinyume cha Qur'an. Akaomba ruhusa ya kufanya jambo alilokwisha fanya tayari. Watu kama hao wanavunja maagizo ya Qur'an, na wanatafuta kufarakisha watu ambao Mungu kwa rehema yake Ameunganisha kwa mkono wa mtu mmoja. Mjihadhari kwao. Tena mtu fulani alisema kwamba nilipoanguka kutoka juu ya farasi jike, hiyo ikamaanisha kuwa nimeanguka kutoka *Ukhalifa*, na kwamba hiyo ilikuwa kwa sababu ya ukosefu wa uimara. Huku ni kuelewa vibaya sana kashfi moja ya Masihi Aliyeahidiwa a.s. Mungu Ameniagiza kuhusu majibu ya hayo yote. Tenganeni na watu kama hao na epukaneni na fikara mbovu"

***Itaendelea toleo lijalo, Inshallah***

# Khuddamul Ahmadiyya yatoa zawadi Temeke hospitali

Siku ya tarehe 26 – 05 – 2012 Tanzeem ya Khuddamul Ahmadiyya Tanzania, katika kusherehekea maadhimisho ya siku ya Ukhalifa yanayofanyika tarehe 27-05-2012 ya kila mwaka duniani kote ilitembelea hospitali ya Manispaa ya Temeke iliyopo mjini Dar es Salaam na kutoa zawadi ya vitu mbalimbali ikiwemo kifaa maalum cha kupimia shinikizo la damu kwa watoto wadogo.

Baadhi ya Viongozi wa Tanzeem hiyo wakiongozwa na Naib Sadr Bw. Seif Hassan Nakuchima walitoa zawadi hizo chini ya utekelezaji wa mpango wa idara ya Tanzeem hiyo inayojulikana kwa jina la Khidmatil Khaliq yaani huduma kwa viumbe waliweza pia kutoa zawadi za biskuti, juisi na sabuni za unga kwa watoto wote waliolazwa wodini hapo wapatao zaidi ya thamanini.

Akipokea zawadi hizo muuguzi mkuu wa zamu wa hospitali hiyo aliwashukuru vijana wa Jumuiya hii kwa kuleta kifaa hicho ambacho kiukweli hakipo hospitalini hapo kwa muda mrefu sasa.

Wakati wakigawa zawadi hizo kwa wagonjwa wote hao Naib Sadr akisaidiwa na Mu'tamad Dr. Pazi Kitabu, Muhtamim Mal Bw. Jafari Sandi, Muhtamim Khidmat Khaliq Bw. Jacob na Bw. Ramadhani Omari ambao aliambatana nao aliwatakia afya njema watoto hao wapate nafuu kwa haraka. Inshallah.



*Naib Sadr Khuddamul Ahmadiyya nchini Tanzania Bw. Seif Hassan Nakuchima akigawa zawadi kwa watoto waliolazwa katika wodi ya watoto kwenye Hospitali ya Mkoa ya Temeke Dar es Salaam wakati yeye na uongozi wengine wa Tanzeem ya Khuddamul Ahmadiyya nchini walipotembelea hospitalini hapo kwa ajili ya kuwapatia zawadi watoto waliolazwa kama sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Ukhalifa duniani tarehe 27 Mei ya kila mwaka.*

Kinamama wote ambao walikuwemo wodini humo wakiwahudumia watoto wao, kwa pamoja walishukuru kwa zawadi hizo kwani ni vitu ambavyo vinawafaa wao na watoto wao pia.

Tanzeem ya Khuddamul Ahmadiyya Tanzania ilitekeleza mpango huo kufuatia kukubaliwa maombi na viongozi wa hospitali hiyo yaliyopelekwa siku chache zilizopita.

Tanzeem ya Khuddamul Ahmadiyya ambayo ni Jumuiya ya vijana hao duniani ilianzishwa siku ya tarehe 4 April, 1938 na Kiongozi wa Jumuiya hii duniani wakati huo Hadhrat Bashiruddin Mahmood Ahmad, ambapo moja ya malengo muhimu ni kutoa huduma kwa viumbe wote wa Mwenyezi Mungu bila kujali itikadi zao na kuendeleza kauli mbiu ya Jumuiya ya Ahmadiyya isemayo "Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote".

# Kigoda cha Mwalimu Nyerere

*Endelea uk. 12*

kampuni hii walipowahi kufanya kazi wanamapinduzi wetu, Mughabuso Mulokozi, Sethy Chachage na Walter Bgoya. Hata ujaze bahari ya maneno kichwa changu bado hakitaelewa unaamuru kutenda mema unasahau nafsi yako?

Jambo la pili ni siku ya mwisho alipoingia tena kwa kishindo, Benjamin William Mkapa, yule mwanafunzi maarufu wa mtu maarufu. Hapana shaka Mkapa kimombo kipo na mimi nalifahamu hilo wakati nilipokutana nae alipokuwa ni rafiki wa familia ya Grant Bwana akifundisha Kiingereza Chang'ombe Chuo cha Ualimu na Janet Grant aliyekuwa ananifundisha Kiingereza shule ya St. Joseph Convent school ya Mjini Dar es salaam. Alieleza mengi akitetea sera zake za ubinafsishaji hoja ambazo niliona ni nyepesi mithili ya manyoya ya kuku!! Nadhani hayo pia ndio yalikuwa maoni ya wasomi waliokuwa wamejaa hadi pomoni katika ukumbi wa Nkurumah. Akimalizia alisema, mtakuwa tayari kuyakabili yatakayotokana na kudiriki kusema hapana kwa wanaoitawala dunia? Na hapo akamkumbuka William Shakespear katika Juliusi Kaisar, "Tatizo halimo kwenye nyota zetu". Nilinuna sana hivi hatuna mshauri au mwandishi wa kuyasema ambayo alilazimika kuyakopa kutoka Kisiwani? Jambo hili si mchezo ndio maana mwanafunzi mwenzie Ngugi wa Thiongo



*Abdulatif Abdallah, b. 1946, Momabsa Kenya*

amejikomboa kwa kuandika katika Kikuyu na kutafuta uhuru zaidi kutoka kwenye mizizi yake.

Sisemi kufahamu Kiingereza ni jambo baya la hasha, si jambo baya, zipo faida zake. Ninachosema tafuta kwanza ufalme wa nyumbani na pakiwa nyumbani hakuna chochote, rukhusa bila shaka ya kwenda kwingineko ipo. Je amejitahidi kupekuwa kutoka kwa Shaaban Robert, Sheikh Kaluta Amri Abedi, Mwinyihatibu Mohamedi, Matias Mnyampala kuwataja wachache.

Kikao cha pili kiliendeshwa katika lugha ya Kiswahili. Eti katika Kiswahili!! Jicho la ubongo wangu lilipanda basi hadi Bungeni Dodoma. Wasomi na wabunge wetu mapacha. Si Kiswahili hicho ni uzungu usio figa wala chungu! Mkulima kutoka Kitonga mwenye mapenzi ya dhati na Nyerere aliniomba nimrudishe nyumbani au nimsindikize hadi kituo cha basi ili aondoke kwani alikuwa amekwisha anza kusikia kichefuchefu. Kuchanganya lugha - Kiingereza kidogo, Kiswahili shabaha yake nini?

Lakini rafiki yangu ameninong'oneza kuwa hata Nyerere alikuwa na kasumba ya kuchanganya Kiingereza na Kiswahili ila kama asemavyo mshairi Mahmood Hamduni, "Huba huficha mengi". Mimi naamini Nyerere hakuwa malaika, kwanini tusikubali yale mabaya akazikwa nayo nasi tukaendelea kuenzi yale mazuri? Washiriki wa Kigoda cha Mwalimu Nyerere kuendelea kuchanganya lugha mbili hivyo ni sunami kwani "Titi la mama" Kiswahili ambacho taratibu zipo dalili kuwa kinashambuliwa na saratani, saratania ya kijana wa kiibo ambaye badala ya kuandika hali ya hewa ya nchi yake akaandika hali ya hewa ya Uingereza!! Viazi ulaya! Kuku wa kizungu!

Licha ya upungufu huo nilipata sururi kubwa kukutana na Abdullatif Abdallah Mshairi huyu maarufu tulifahamiana miaka ya 70 wakati nikifanya kazi Printpark yeye alikuwa anakuja kiwandani hapo ili kuchapisha baadhi ya kazi za Taasisi ya Uchunguzi wa lugha ya Kiswahili. Tulikuwa tukizungumza mengi na alipenda sana kusoma mashairi ya Sheikh Kaluta Amri Abedi.

Aliwahi pia kunipa utenzi wake wa Adam na Hawa, nilipokwisha usoma utenzi huo tulikuwa na mazungumzo nikamueleza itikadi ya Ahmadiyya inavyoamini kuwa Adam (as) hakuwa mtu wa kwanza kuumbwa isipokuwa Nabii wa kwanza kuanzisha utamaduni na ustaarabu licha ya tofauti zetu hakukasirika.

Wakati wa mapumziko aliniona na akaja tukakumbatiana kwa dakika na akaonesha furaha kubwa sana. Watu walishangaa huyu anafahamiana vipi na mshairi maarufu ambaye ametoa diwani *'Sauti ya Dhiki'* na kuwa Mhariri wa *African Events.* Nilimwambia wakati tumekumbatiana ya kwamba mara baada ya kuwasilisha nilikumbuka ubeti wa Sheikh Kaluta Amri Abedi:

Safari nimesafiri,
nti nyingi nifikile
Sijaipata sururi,
ja mvita inipele
Inao wana wa ari,
wazuri wana wapole.

Alifurahi sana. Kufikia umaarufu huo na akaendelea kutukumbuka sisi pangu pakavu weka mchuzi. Ni ufaulu mkubwa na kielelezo cha usafi wa moyo.

Ngoja nikope maneno ya Sheikh Kaluta Amri Abedi

Bwana wewe mfadhili,
unazo busara tele
Cha Madaraka kivuli,
kikufunike milele
Mwasifiwa tangu kale,
enyi wana wa Mvita.

# Falsafa ya safari ya Mbali - Miiraj

*Kutoka uk. 12*

huyu mpenzi wa Subhana Wata'ala hadi kwake". Buraku akamjibu Jibril: "Naam, nipo twayari kuifanya kazi hiyo bila wasi wasi wowote hiyo ndiyo shughuli niliyojiya hapa. Mimi pia ninahitaji baraka na pepo ya Allah".

Hapo Buraku akamwita Mtume (saw) kwa furaha na bashasha. Akamwambia; "Nipo twayari kukutumikia ewe Mtume wa Mungu". Buraku akainika kichwa chake chini kisha Mtume (saw) akampanda juu yake. Kabla hawajaondoka Mtume (saw) akaomba dua kwa Mwenyezi Mungu ili safari iwe ya salama usalimini. Safari ilikuwa ya watatu: Malaika Jibrilu, Mtume Muhammad (saw) na Buraku. Safari ilianzia Makkatul-Mukarram hadi Madinatul-Munawwar. Hiyo ikiwa ni hatua yao ya kwanza. Seyidna Jibril ndiye kiongozi wa msafara huu. Naam, walipofika Madina, Jibril akamwambia Mtume (saw), "haya shuka hapa kisha umuombe sana Rabbi. Swali rakaa mbili kwa utii na unyenyekevu mkubwa"

Baada ya kuambizana hayo na Mtume (saw) kutekeleza, msafara wao ulielekea kwenye mlima Sinai. Seyidna Jibrilu akamwambia Mtume (saw) "Hapa piya usali ewe Mtume wa Mungu. Hapa ni mahali patakatifu ambapo Nabii Musa bim Imran (as) alizungumza na Mwenyezi Mungu". Mjumbe wa Allah akafanya kama alivyoambiwa. Basi toka hapo msafara ulifika Bethelehemu ambako Isa (as) mwana wa Mariam alikozaliwa. Seyidina jibrilu akamwambia tena Mtume (saw) "Haya hapa pia swali na umuombe sana Mwenyezi Mungu kwa sababu ni mahali patakatifu. Hapa ni pale ambapo Seyidna Isa (as) amezaliwa". Seyidna Muhammad (saw) akafanya kama alivyoambiwa.

Baada ya hapo, waliondoka Bethelehemu wakiendelea na safari yao. Naam, walifika mahali fulani wakawaona viumbe wanaoitwa majini. Majini ni viumbe wasioonekana kwa haya macho yetu. Majini hao walikuwa wameshika mikononi mwao vijinga vya moto vikimmulika Mtume Muhammad (saw). Seyidna Jibril akaitowa kauli kumwambiya Mtume (saw), "Omba duwa, omba sana kwa Wadudi". Basi, Mtume (saw) akaomba mara yale majini yakatoweka.

Wakaendelea na msafara wao huku wakiona mambo mengi ya ajabu wapitamo. Sehemu fulani waliona watu wakilima na kupanda mashamba yao na siku hiyo hiyo, bali wakati huo huo walikuwa wanavuna mazao mengi sana. Seyidna Jibril akamweleza Mtume Muhammad (saw) kwamba watu hao ni wale Mujahidina. Ni wale watu wafanyao jihadi ya kila aina katika njia ya Mwenyezi Mungu. Allah, Subhana wata'ala Atawalipa mema papo kwa papo bila kuchukuwa muda.

Kisha wakaendelea mbele na safari yao. Mara wakasikia harufu nzuri ikinukia. Jibril akamweleza Mtume Muhammad (saw), "Hiyo ni harufu ya mke mwema ambaye alikuwa anachana nywele za mwanamke asiye na huruma ambaye ni bintiye Firauni. Mtume (saw) akamuona Firauni akikusanya mke, wanawake, wana na mabinti wote na kuwatia ndani ya sufuria yenye mafuta ya moto. Hiyo ndiyo harufu njema inukiayo ya watu wema.

Wakaendelea na safari yao hadi walipowaona watu wakipondaponda vichwa vyao kwa nyundo za chuma. Seyidna Jibril akamwambia Mtume Muhammad (saw) kwamba asishangae sana kwani hao awaonao ni wale watu ambao wavivu katika kuswali swala tano. Bali walipoendelea kwenda mbele kidogo wakawaona watu wengine. Hawa wamevaa marapurapu na nguo zilizochanikachanika na huku zingine zimetiwa viraka.

Seyidna Jibril akamwambia MtumeMuhammad(saw),"Hao ni wale watu ambao si wema. Hawatoi Zakka wala sadaka, bali mali zao wanalimatia. Ni wale wanaofanya ubakhili katika kutoa kwa njia ya dini ya Mwenyezi Mungu".

Wakasonga mbele kuendelea na safari yao. Wakafika mahali wakawakuta watu wanakula nyama mbichi huku madamu yakichuruzika wakiacha iliyopikwa na kuiva vyema. Jibril akamwambia Mtume (saw) wale watu awaonao ni watu wanaume na wanawake ambao ni wazinzi. Kisha wakaenda hatua chache wakakuta mti umekingikwa njiani nao unapasuwa nguo ya kila apitaye mahala hapo, wala hayupo aliyesalimika. Jibril akamwambia Mtume Muhammad (saw), hao ndiyo wale watu wanaoishi kandokando ya mabarabara na njia halafu hawatowi haki ya mapito hayo. Basi jazaa yao watu hao ni jahanamu.

Kutoka hapo wakaenda mbele na huko wakaona mto wa damu na ndani yake mlikuwa na watu wanaishi, bali chakula chao walichokuwa wanakula ni sumu. Jibril akamweleza Nabii Muhammad (saw) kwamba hao ni watu wale wanaokula vitu vya kharamu, na hiyo ndiyo jazaa yao siku ya kiyama. Kwa mbele kidogo wakamuona mtu mmoja dhalili sana ambaye hana siha njema. Pamoja kuwa katika hali hiyo, bado alikuwa anajitwisha mizigo mizito. Huu baada ya huu. Alikuwa anaongeza mizigo baada ya mwingine. Seyidna Jibril akamueleza Mtume (saw) kwamba mtu huyo ni katika wale watu wanaokula amana za watu wanapokabidhiwa wazitunze.

Walipotoka hapo wakaendelea mbale na huko wakaona watu wengine. Hao walikuwa wanakatwa ndimi zao kwa mikasi, kisha zinarejea tena kama kwanza. Jibril akamwambia Mtume (saw) kwamba hao ndiyo wale wote wasemao maneno ya batwili. Ni wale waongo ambao hawasemi kweli. Baada ya hapo wakaona watu wengine wakijiparura nyuso zao kwa mikucha yao. Jibril akamweleza Mtume (saw) kuwa hao ni watu wabaya ambao siku ya kiyama nyuso zao zitakuwa hazina nyama.

Wakaendelea mbele ndipo wakaona ng'ombe anatoka kwenye tundu dogo kama kunazi, lakini ng'ombe huyo hawezi tena kurejea katika tundu hilo. Jibril akanena kumwambia Mjumbe wa Mungu Muhammad Mustafa (saw) kwamba hali ya namna hiyo ni ya wale wasemao maneno wasomaizi na khatimaye kujiuma kidole na kujuta, ole wao.

Msafara ukaendelea, sasa wakafika mahala fulani ambapo waliona wangwa tawili. Sauti nzuri ilisikika na harufu njema ilisambaa. Seyidna Jibril akamtaarifu Muhammad (saw) kwa kusema, "Ewe Mtume wa Mungu, sikiliza swauti ya pepo inavyovuma. Pepo hiyo inasema; "Ee Rabbi, Mola wangu, nawataka watu wangu, nina hamu kubwa kuwaona. Neema nyingi imeandaliwa kwa ajili yao. Ah! Lini watakuja"

Baada ya kuoneshwa hayo, wakaenda kidogo mbele. Hapo wakaona wangwa mwingine wa hari, wenye swauti mbaya na ya kutisha. Ni swauti kama ile ya punda. Harufu mbaya mno ilisikika. Hayupo anayeweza kustahamili kuvuta hewa yake. Jibril akamwambia Seyidna Muhammad (saw) kuwa hiyo ndiyo swauti ya Jahanamu. Hapo Bwana wetu Muhammad (saw) hakustahamili, bali akasema "Yaa Rabbi, nasikitishwa na huu moto uunguzao, ninaomba nusura kwa ajili ya watu wangu, kwa sababu wengi wao ni watu wa Jahanamu".

Walipoondoka hapo, wakaendelea na msafara wao. Wapo hapa. Hapo sasa waliona nguzo ya nuru imechukuliwa juu, juu zaidi. Jibril akasema, "Ewe Mjumbe wa Allah, yakuupasa ukariri na kukumbuka kwamba nguzo ya Imani iwekwe chini ya mbingu". Baada ya maelezo hayo mara wakasikia swauti ya tangazo. Kulikuwa na mnadi, Mtume Muhammad (saw) akanyamaa kimya kusikiliza tangazo. Hakunyanyua kinywa wala hakutikisika. Lakini Seyidna Jibril akamsemesha kwa kumwambia huyo aliye kuwa akinadi ni nani. "Ewe mtoto, wewe ni Myahudi tu ijapokuwa unatisha kiasi hicho kwa sauti yako". Kisha akajitokeza mtu mmoja mwingine mwenye machachari na mambo ya kutisha. Mtume (saw) akakaa kimya vilevile. Seyina Jibril akamwambia Mtukufu Mtume Muhammad (saw) kwamba mtu huyo ni Mkristo asiye na chochote wala lolote, ila shabaha yake anataka kuwapoteza watu wako wote kwa kuwatowa kwenye njia iliyonyooka na kuwapeleka kwenye upotevu.

Toka hapo wakaenda mbele, wakamuona mwanamke mzuri kweli kweli. Amevaa libasi ya utanashati. Amejivisha kholia za tafakhuri huku akionesha wema na ihisani. Seyidna Jibril akasema kumwambia Mja wa Allah, Muhammad (saw) hivi, "Dunia yenu hii ni bibi arusi, inapendezesha na mara zote inaghururisha wakaaji wake"

Naam, wakaendelea na safari yao. Hapa sasa wanakutana na mtu mmoja shaibu. Bwana mkubwa huyo akitaka kuzungumza na Mtume (saw), lakini Mtume (saw) hakusema naye chochote wala hakujibu kitu. Ndipo Jibril akasema, "Ewe Muhammad Mja wa Mungu, umetenda vyema sana kutozungumza na huyo bwana. Huyo ni adui yako. Huyo ni adui wa umati wako pia. Huyo ndiye yule aitwaye Ibilisi maluuni".

Kutoka hapo msafara ukafika sehemu moja ambako hapo wakaona mitume wote waliopita zamani. Mitume hao kwa pamoja walimsalimu Mtukufu Seyidna Muhammad (saw) toka hapo Seyidna Jibril na Mtume (saw) wakafika nyumba kuu na moja kwa moja wakaingia ndani. Hapo ni Baitul Mudaddasi, ndipo mahali paitwapo nyumba kuu. Naam, wakaingia katika Msikiti wenye baraka na amani. Wakaona nuru na jaha mbili zikimetuka. Moja upande wa miharabu ya Daudi na ya pili ni nuru za kaburi ya mama-Mariyamu.

Baada ya hapo, Seyidna Jibril akasimama wima na kutowa Adhana kwa swauti sana. Mara mitume wote wa zamani wakakusanyika pale Msikitini. Seyidna Adam na Nuhu. Lut na Ibrahimu, Ismail na Isihaka, Seyidna Zakariya, Yakubu na Yusufu. Nabii Swaleh, Daudi na Suleimani. Seyidna Lukuman, Shuwaibu, Ilyasa, Yunusu na Ayubu. Dhulkifli, Yahya na Yunusu. Nabii Idrisa, Nabii Musa na Isa mwana wa Mariayamu ni miongoni mwa mitume waliiokusanyika hapo kwa ajili ya swala. Basi Seyidna Jibril akakimu na wale manabii bila kufahamu Imamu atakuwa nani. Lakini Jibril akamtanguliza Muhammad (saw) na kusema, "Haya tangulia ewe Muhammad. Wewe ndiwe Imamu wetu na Mitume wote wako nyuma yako. Tafadhali, takadamu. Maana saada ni yako. Heshima na taadhima ipo juu yako, kwani wewe ndiwe mteule na mwombezi wa watu na viumbe vyote".

Baada ya kumaliza kuswali, kila mtu akamdhukuru Mwenyezi Mungu kwa sifa zake njema.

Hapa ndipo iliposhuka MIIRAJI ambayo imepambwa kwa fedha, almasi, dhahabu na marijani. Seyidna Jibril na Mtume (saw) wakapanda hadi mbinguni.

Seyidna Jibril na Seyidna Muhammad (saw) wakaingia mbinguni, wakabisha hodi kwenye mlango mara watu wa samai wakaitikia wakiuliza, "U nani wewe mwenye nuru namna hii ambayo imeeneya kila upande" Seyidna Jibril akajibu na kuwaambia kwamba aliyegonga mlango ni Muombezi wa ulimwengu, mtukufu Mtume Muhammad (saw), mfungulieni mlango aingie. Basi wakafunguliwa mlango kwa hima hima tena kwa heshima na taadhima.

Hapo ndipo Seyidna Muhammad (saw) alipomuona Babu yetu Adamu. Basi, Seyidna Muhammad akamsalimu Nabii Adamu. Seyidna Adamu akaitikia kwa huba na mapenzi makubwa. "Marahaba mwana mwema ewe Mtume wa Mungu. Wewe ndiwe wa awali, ndiwe wa mbele na Mitume wote wako nyuma yako".

Walipotoka hapo wakaelekea mbingu ya pili. Nako wakabisha hodi pia wakaitikiwa kama walivyoitikiwa mbingu ya kwanza. Naam, hapo walimuona Nabii Isa (as) na Nabii Yahya ambao sura zao zilifanana sana kana kwamba ni wana wa baba na mama mmoja, bali kama mapacha vile! Mtume (saw) akawatolea salaam kwa heshima nao pale walipokaa wakainuka na kusimama kumlaki Seyidna Muhammad (saw), Mtume wa Mwenyezi Mungu kipenzi chake. Hawakuweza kuzungumza sana, mara wakaachana. Jibril na Seyidna Muhammad (saw) wakaendelea na msafara wao hadi mbingu ya tatu. Kama kawaida wakabisha hodi kwa adabu, nao wakaitikiwa kwa kustatwii. Kwenye uwingu huu walimuona Seyidna Yusuf mwenye sura jamili ajabu. Hajapata kutokea! Basi wakamtolea salamu. Baada ya kuitikiwa kama sheria inavyosema, walikaribishwa kwenye sehemu muhimu.

***Itaendelea toleo lijalo, Inshallah***

# Dhati ya Seyyidna Ahmad

*Kutoka uk. 12*

na kwamba kama atapata kukutana naye basi ataibusu miguu yake. Malik sahib anasema kwamba baada ya kufanya baiat alimuona kwa macho yake Sahibzada shaheed akiibusu miguu iliyobarikiwa ya Masihi Aliyeahidiwa a.s.

Hadhrat Maulwi Sakandar Ali sahib r.a.: Anasimulia kwamba katika safari zake za Qadian kabla ya kuamua kuhamia moja kwa moja alikwenda kwenye matembezi ya asubuhi pamoja na Masihi Aliyeahidiwa a.s. Anakumbuka Masihi Aliyeahidiwa a.s. alisema kwamba mtu ambaye hawezi kuacha mambo madogo madogo kama vile kuvuta sigara na vileo vingine, mambo ambayo kwa kuyaacha hapati kumuudhi mtu yeyoye, inawezekanaje mtu huyo aweze kuyawacha mambo makubwa ambayo yatawafanya hata watu wake wa karibu wawe dhidi yake? Maulvi Sahib anaandika kwamba wakati huo alikuwa ni mvutaji kileo aina ya Hookah lakini mara tu aliposikia kauli hiyo ya Masihi Aliyeahidiwa a.s. akafanya maamuzi ya kuwacha mara moja. Bila shaka ilikuwa ni mapenzi yake na kujitolea kwake kwa Masihi Aliyeahidiwa a.s. ndiko kulikomfanya aweze kuachana na kileo hicho.

Hadhrat Shukr Elahi Ahmadi r.a.: Anasimulia wakati akiwa na umri wa miaka kumi na mbili na akiwa hana habari yoyote ya dini; Masihi Aliyeahidiwa a.s. alikuwa akifika mahakamani karibu na shule aliyokuwa akisoma. Yeye alikuwa akikimbia shuleni ili apate nafasi ya kuuona uso uliobarikiwa wa Masihi Aliyeahidiwa a.s.. Alikuwa akishangazwa mno na sahaba mmoja wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. ambaye alikuwa akibeba feni kubwa kwa mkono wake wa kulia na alikuwa akimpepea Masihi Aliyeahidiwa a.s. kwa nguvu kana kwamba feni hiyo iliendeshwa kwa umeme. Akiwa mtoto alikuwa akishangaa maajabu hayo ya kujitolea kwa jazba ya sahaba huyo wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. kwa kumpepea kwa mkono mmoja. Anaandika kwamba sasa ameelewa kuwa ilikuwa ni mapenzi na kujitolea kwa sahaba huyo mbele ya Masihi Aliyeahidiwa a.s. kulikomfanya amtumikie hivyo.

Hadhrat Madad Khan sahib r.a.: Anasimulia alikuwa amejiunga na jeshi na alipenda kutembelea Qadian kabla ya kaunza kazi yake hiyo ili apate nafasi ya kufanya Baiat kwa mkono wake kwani kabla alikuwa amefanya baiat kupitia barua. Alihofia kama atakwenda kwenye ajira moja kwa moja huenda baadae akakosa nafasi ya kumuaona Masihi Aliyeahidiwa a.s.. Alipofika Qadian na kumuona Masihi Aliyeahidiwa a.s. alijhisi kwamba hata kama angepewa Kashamir yote hangekuwa tayari kuondoka Qadian. Kwa kuuona uso uliobarikiwa wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. ilikuwa ni vigumu mno kwake kuondoka Qadian. Alisahau kila kitu na akajisemea kwamba hata kama angelilipwa mshahara wa maelfu ya rupia lakini awe nje ya Qadian fedha hizo hazitokuwa na thamani yoyote.

Hadhrat Muhammad Ismail sahib r.a.: Anasimulia yeye akiwa na umri wa miaka 20 Masihi Aliyeahidiwa a.s. alitembelea Gurdaspur kwa ajili ya kuhudhuria kesi mahakamani. Ismail sahib alifika kumuona Masihi Aliyeahidiwa a.s. akiwa amefuatana na baba yake pamoja na watu wengine. Ismail Sahib akapata nafasi ya kumpepea Masihi Aliyeahidiwa a.s.. Masihi Aliyeahidiwa a.s. akiwa na tabasamu alimuelekea baba wa Ismil Sahib na kumwambia "Mian Ismael amejipatia sehemu yake ya thawabu. Ismail Sahib anasimulia kwamba kila wakati alipolikumbuka tukio hilo alijisikia mwenye furaha mno.

Hadhrat Sheikh Asghar Ali sahib r.a.: Anasimulia kwa kawaida marafiki waliomtembelea Masihi Aliyeahidiwa a.s. walipokuwa wakiaga kuondoka Qadian Masihi Aliyeahidiwa a.s. alikuwa akiwasihi waendelee kutembelea mara kwa mara. Wakati mwingine Masihi Aliyeahidiwa a.s. alipoona watu wanaweza kubaki siku nyingi zaidi alikuwa akiwasihi wazidishe siku zaidi za kubaki Qadian. Kila mgeni alikuwa akiondoka Qadian baada ya kumuomba Masihi Aliyeahidiwa a.s. pamoja na kuagana naye kwa kupeana naye mkono. Baadhi ya wakati kupeana mikono kulichukua muda mrefu kiasi kwamba ilijitokeza hofu ya kuchelewa kufika kituo cha reli kwa wakati. Asghar sahib anasimulia kwamba hali hiyo ilitokea kwake mara kadhaa pia. Mara zote walikuwa wakiharakia kufika kituo cha reli ili wawahi lakini kila mara waliikuta treni bado haijafika.

Hadhrat Master Nazir Hussein sahib r.a.: Anasimulia kwamba ilikuwa ni tabia yake ya kudumu kila mara alipopata bahati ya kuwa pamoja na Masihi Aliyeahidiwa a.s. alihakikisha kwamba anakuwa na taftari la kutunzia kumbukumbu (note book) pamoja na kalamu ili apate kuandika jambo lolote atakaloagizwa na Masihi Aliyeahidiwa a.s. kulitekeleza.

Hadhrat Allah Ditta sahib r.a.: Anasimulia mnamo 1901 au 1902 Nawab sahib alifika kwa Hadhrat Maulana Nur ud din kwa ajili ya matibabu yeye na wafanyakazi wake wachache. Nawab sahib alipenda kwamba atakaporudi mjini kwake arudi pamoja na Hadhrat Maulana Nur ud din. Lakini alipomweleza matakwa yake Hadhrat Maulana Nur ud din akamwambia kwamba yeye anaye bwana wake ambaye kama atamruhusu kwenda naye basi atakwenda vinginevyo hawezi kufanya maamuzi ya kwake mwenyewe. Hivyo akamtaka Nawab Sahib aongee yeye mwenyewe na Masihi Aliyeahidiwa a.s.. Nawab sahib akawatuma watumishi wake wakaongee na Masihi Aliyeahidiwa a.s. ambaye aliwajibu kwamba kwa hakika hakuna shaka yoyote kuwa iwapo 'nitamwagiza Maulvi sahib ajitupe kwenye moto au azame chini ya maji basi atafanye hivyo, lakini anahitajika sana hapa Qadian kwa ajili ya kuwatibu watu maskini na wanyonge, hivyo iwapo Nawab sahib anataka kupata huduma zake za kitibabu hana budi aendelee kubaki Qadian'.

Hadhrat Maulana Nur ud din r.a. aliposikia jinsi Masihi Aliyeahidiwa a.s. alivyoongea juu yake alijawa na furaha sana na akasema kwamba furaha aliyoipata kuhusu jinsi bwana wake anavyomfikiria ni ya kiasi hiki kwamba hajui aielezee kwa maneno gani.

Hadhrat Master Maula Bakhsh sahib r.a.: Anasimulia mara moja aliwahi kutembelea Qadian katika siku zake za likizo. Baada ya siku chache alipoamua kurudi kwao akiwa njiani alishindwa kuendelea mbele na safari na akabaki kwenye mashamba akiwa analia. Akaamua kurudi Qadian na akabaki huko mpaka likizo yake ilipoisha.

Hadhrat Haji Musa sahib r.a. anasimulia kwamba siku moja mtoto wake mwenye umri wa miaka minne alianza kulia na kudai kwamba lazima apelekewe kwa Masihi Aliyeahidiwa a.s. ili akumbatiane naye. Mtoto huyo akasisitiza dai lake hilo kwa nguvu. Siku iliyofata Musa sahib alisafiri kwa treni akiwa na mtoto wake hadi Qadian. Alipofika Qadian ujumbe ukatumwa kwa Masihi Aliyeahidiwa a.s. kwamba kuna mtoto mwenye shauku ya kukumbatiana naye. Mara tu Masihi Aliyeahidiwa a.s. alipotokea mtoto yule aliikumbatia miguu yake na kusema kitoto kwamba sasa nimeridhika.

Hadhrat Sheikh Zainul Abideen sahib r.a.: Anasimulia kwamba kaka yake ambaye alikuwa ni mwanafunzi wa darasa la nane aliugua sana. Matumaini yote ya kupona yalipofutika wakampeleka Qadian. Baada ya maombi, Masihi Aliyeahidiwa a.s. alipata ufunuo kwamba mtoto yule hatopona. Hivyo akamuomba baba wa mtoto huyo arudi naye nyumbani kwani wahyi unaonesha kwamba hatopona. Hata hivyo baba yake akakataa kumrudisha na akasema iwapo atafariki Qadian basi atapa baraka ya kusaliwa na Masihi Aliyeahidiwa a.s.. Jioni moja mtoto yule alifariki. Masihi Aliyeahidiwa a.s. akaongoza sala ya jeneza. Sala hiyo ya jeneza ilikuwa ndefu ikimuacha kila mtu taabani.

Hadhrat Mian Abdur Razzaq sahib r.a anasimulia kwamba anakumbuka mara moja Masihi Aliyeahidiwa a.s. alipotembelea Jhelum kwa ajili ya kesi mahakamani jinsi watu walivyokusanyika ili wapate kugusana naye. Watu waliotaka kugusana naye walikuwa ni wengi kiasi hiki kwamba ililazimika polisi kuingilia kati. Mian Sahib anasimulia kwamba wao hofu yao kubwa ilikuwa ni juu ya usalama wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. na wakatulia alipofika kwenye makazi yake salama.

Hadhrat Mian Wazir Muhammad Khan r.a.: Anasimulia kwamba mara ya kwanza macho yake yalipoanguka juu ya uso uliobarikiwa wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. fahamu zake zilichanganyikiwa. Alisali sala ya Ijumaa karibu na Masihi Aliyeahidiwa a.s. na akabaini kwamba Masihi Aliyeahidiwa a.s. amemuangalia kwa jicho la umakini. Hali hiyo ilimgusa sana kiasi hiki kwamba muda wote wa sala alibaki akilia kwa kwikwi na akaendelea kulia hata baada ya sala.

Hadhrat Dr Ghulam Ghaus sahib r.a. anaandika kwamba Mir Mehdi Hussein anasimulia kwamba wakati fulani alitumwa kutoka Qadian kwenda Amritsar kununua barafu. Wakati akirudi akatoa kichwa chake nje ya dirisha la treni na kofia yake ikadondoka. Alipofika Qadian Mir Nasir Nawab akamuuliza nini kilichomkuta, je amepigwa, mbona alikuwa hana kofia. Akajibu kofia yake ilipeperushwa na upepo. Mir Nasir Nawab sahib akamsimulia tukio hili Masihi Aliyeahidiwa a.s. ambaye alisema kwamba atampatia kofia nyingine. Mir Mehdi mwenyewe binafsi hakuwa na dai hilo na kajinunulia kofia ya kawaida tu. Baada ya kipindi kama miezi sita Masihi Aliyeahidiwa a.s. alimpatia kofia, koti na viatu. Mwenyewe akatumia kofia na koti na kumpatia viatu baba yake. Wakati akirejea kwao mtu mmoja akamwambia kwamba kofia yake inaonekana kongwe na iliyokwisha kutumika na akamuahidi kumpatia kofia kutoka Amritsar. Mir Mehdi akamjibu kwamba kofia kama hiyo haiwezi kupatikana mahala popote ardhini wala mbinguni kwa sababu ni kiofia iliyowahi kuvaliwa na Masihi Aliyeahidiwa a.s. kwa miaka kadhaa.

Hadhrat Maulwi Aziz Din sahib r.a.: Anasimulia kwamba yeye amewahi kukutana na Masihi Aliyeahidiwa a.s. zaidi ya mara sitini au sabiini. Kila mara alipokutana na Masihi Aliyeahidiwa a.s. alivua kilemba chake na kuichukua mikono ya Masihi Aliyeahidiwa a.s. na kuisugulia kichwa chake. Wakati akifanya hivyo Masihi Aliyeahidiwa a.s. alikuwa kimwacha na hakuna siku aliyomzuia hata kama ametumia muda mrefu kiasi gani hadi pale alipoiachia mikono yeye mwenywe. Aziz sahib anasimulia kwamba matokeo yake aliishi umri wa miaka (81) themanini na moja na hakuwahi kuugua hata mara moja.

Hadhrat Muhammad Zahoor ud din sahib r.a.: Anasimulia kwa mara ya mwisho kuitembelea Qadian, Masihi Aliyeahidiwa a.s. alipofariki ilipita miezi minne ndipo wao wakapata habari za kifo chake kwamba alifariki akiwa safarini mjini Lahore. Anasimulia kwamba baba mkwe wake alikuwa pamoja naye kwenye huzuni hiyo. Walikimbilia kituo cha treni ili kutuma Telegramu Lahore kuulizia juu ya ukweli wa taarifa hizo. Walikimbia bila kuvaa viatu, wasio Waahmadiyya walipowaona hivyo wakaanza kuwacheka na kuwadhihaki lakini wao hawakujali kwani kwao huu ulikuwa ni msiba mzito sana. Baada ya kupata taarifa kwamba Hadhrat Khalifatul Masih I amechaguliwa wakatuma baiat zao kwake na mwishoni mwa mwaka wakahudhuria Jalsa Salana ya Qadian. Kwenye Jalsa Mian Mahmood r.a. alitoa hotuba ambamo ndani yake akasema machozi ya wana wa Israeli ndiyo yaliyobadilika kuwa bahari iliyomuangamiza Firauni. Hotuba hii ilimuacha kila moja katika hali ya tafakuri kubwa. Baadae ikafuata hotuba ya Hadhrat Khalifatul Masih I r.a. ambaye kabla ya kutoa hotuba yake akasema Mian Mahmood ameongea juu ya mada ambayo haijawahipo kunipitia kwenye mawazo yangu.

Hadhrat Sheikh Muhammad Ismail sahib r.a. anasimulia kwamba mtu kusali ndani ya Masjid Mubaraka anapata hisia za kiroho na hofu ya Mwenyezi Mungu lakini kwa kukosekana 'Nuru ile ya Mungu' (Masihi Aliyeahidiwa a.s.) mtu anajawa na huzuni na kwa kukumbuka baraka za kuwa pamoja naye moyo wa mtu unajaa maumivu. Mtu alikuwa anasahau matatizo yake yote kwa kuangalia tu 'nuru ile ya Mungu' na kwa kuwa pamoja naye ilikuwa kana kwamba mtu yumo peponi. Anasimulia kwamba walijawa na mapenzi ya Masihi Aliyeahidiwa a.s. kiasi hiki kwamba vijana baada ya kusali sala moja walikuwa na hamu sala nyingine ifike ili wapate nafasi ya kusali karibu na Masihi Aliyeahidiwa a.s.. Dhati yake ilibarikiwa kiasi hiki kwamba wafuasi wake waliisahau dunia. Alikuwa amewafikisha kwenye kizingiti cha Mungu.

Hadhrat Khalifatul Masih a.t.b.a. akaomba kwamba nasi pia tuwezeshwe kutimiza matakwa ya Baiat na tupewe nguvu ya kuonyesha mapenzi na utii kwa Masihi Aliyeahidiwa a.s. ili kwamba tuweze kumtumikia Mtume Mtukufu Muhammad s.a.w. kwa ukamilifu.

**Mwisho.**

The First Muslim Newspaper in Kiswahili Language since 1936

# Mapenzi ya Mungu

Rajab 1433 AH | Mei 2012 | Hijrat 1391 HS

**Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu s.a.w**

**Imesimuliwa na Hadhrat Safina r.a. ya kwamba Mtume s.a.w. alisema: Ukhalifa utakuwa kwa miaka thelathini. Kisha baadaye ufalme utapatikana .... (*Musnad Ahmad*)**

# Dhati ya Sayyidna Ahmad a.s. ilikuwa na nuru iliyowavuta Masahaba zake - Khalifa Mtukufu

Kwenye hotuba ya Ijumaa ya tarehe _____ Huzur a.t.b.a. alisimulia matukio kadhaa yanayoonesha mapenzi na utii wa masahaba wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. kwake.

Katika sharti la kumi la Baiat Masihi Aliyeahidiwa a.s. amesema kwamba mahusiano ya kidugu na utii kwake yanatakiwa yashinde mahusiano mengine yote ya kidunia. Jambo hili ni la lazima kwani katika zama hizi yeye ndiye mtumishi mwenye jazba na uaminifu zaidi kwa mtukufu Mtume s.a.w., ambaye sawa na bishara za Mtukufu Mtume s.a.w. ameileta tena imani ambayo ilikuwa imepanda kwenye vilimia, ameisafisha dini dhidi ya bidaa zilizoidhuru na ameionesha dunia mafundisho safi ya Islam. Kwa msingi huo amedhihirisha ukweli wa cheo cha Mtukufu Mtume s.a.w. na maungano kati ya mja na Mungu.

Masihi Aliyeahidiwa a.s. amesema: Ninajua kutokana na uzoefu wangu uliohakikika na kwa elimu iliyokamilika kwamba hakuna mtu yeyote leo awezaye kumfikia Mungu wala kupata elimu ya kweli ya kiroho bila ya kuwa mfuasi wa Mtukufu Mtume s.a.w.



*Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s , Masihi Aliyeahidiwa na Imam Mahdi*

Utii wa Masihi Aliyeahidiwa uliokamilika na uliohalisika kwa Mtukufu Mtume s.a.w. ndio uliokuwa chanzo cha yeye kupata ukaribu na Mwenyezi Mungu, Naye Mwenyezi Mungu akaamua iwe lazima kudumisha uhusiano wa kidugu na utiifu kwa Mwasihi Aliyeahidiwa a.s.

Masihi Aliyeahidiwa amesema kwamba wakati mtu anapompenda Mwenyezi Mungu kwa mapenzi ya kweli Mwenyezi Mungu naye humpenda sana mtu huyo. Kukubaliwa kwa maombi huunganishwa na mtu huyo na mapenzi yake hujazwa kwenye maelfu ya nyoyo za watu na pia huruzukiwa mvuto wenye nguvu. Mtu huyo hushushiwa nuru ambayo hubaki pamoja naye daima.

Hadhrat Allah Yar sahib r.a: Anasimulia kwamba kutokana na mapenzi yake ya juu kabisa ya kujitolea kwa Masihi Aliyeahidiwa a.s. alihamia Qadian na akaanzisha kazi ya uchongaji. Mapato yake yakapungua sana na ili aweze kukidhi mahitaji ya maisha ilimbidi pia anunue tamtam na kuziuza. Alijenga kijibanda chake cha kufanyia biashara kwa chini akielekea moja kwa moja mlango wa nyumba ya Masihi Aliyeahidiwa a.s. Siku Moja Hadhrat Amaan Jan r.a. akimsikia akinadi biashara yake kutoka nje, kwa sauti ya juu alimweleza Masihi Aliyeahidiwa a.s. kuhusu maamuzi ya Allah Yar sahib ya kufanya biashara yenye mapato madogo kama hiyo na akashauri iwapo kama anaweza kufanya biashara nyingine na Masihi Aliyeahidiwa a.s. akaeleza kubanwa kwa Allah Yar Sahib alikonako. Wakati huo Allah Yar Sahib akapata kuyasikia mazungumzo hayo kutokea upande wa chini. Baadae Masihi Aliyeahidiwa a.s. akampatia agizo la kumtengenezea vitanda ishirini kwa malipo kwa aina yoyote ya mbao atakayomudu kuipata.

Hadhrat Malik Khan Sahib: Anasimulia kwamba alitembelea Qadian akiandamana na Sahibzada Abdul Latif shaheed r.a. na huenda ikawa ni siku ya pili tu baada ya kufika huko alichukua Baiat. Baadae walibaki Qadian kwa siku chache. Malik Sahib anasimulia kwamba Sahibzada shaheed alikuwa akisema kwamba hajawahipo kukutana na mwanaulama mkubwa kumshinda yeye mwenyewe

*Endelea uk. 11*

# Falsafa ya safari ya Mbali - Miiraj

**Na Ustadh Khamisi Wamwera, Mbagara rangi 3 Dar es salaam**

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema na Mwingi wa Ukarimu. Ewe Mola wangu mrehemu Muhammad (saw) na wafuasi wa Muhammad (saw) kama ulivyomrehemu Ibrahimu na wafuasi wa Ibrahimu (as). Wabariki hao na uwape salama na amani, maana Wewe Ndiye Mwenye uwezo juu ya kila kitu.

Naam, ninatarajia kuweka mbele yenu maelezo ya safari ya Miiraji ya Mtukufu Mtume Muhammad (saw). Maelezo haya ni kama yalivyoandikwa katika swahifa mbalimbali za wanazuoni wakubwa wa dini ya Iislam, wanaanza kwa kusema;

Ni Khadithi njema ya usiku wa Miiraji. Katika usiku huo, Mwenyezi Mungu Azza wajalla Alionesha jaha na uwezo wake mkubwa alio nao.



*Al Ustadh Khamis Wamwera*

Masimulizi yanasema kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu siku hiyo alimshusha Seyidna Jibril (as) hadi ardhini. Kufumba na kufumbuwa akafika nyumbani kwa Mtume (saw) akiamkuta amelala. Seyidna Muhammad (saw) siku ile alikuwa amelala nyumbani kwa bibi Aisha (ra). Jibril akamwamsha Mtume Muhammad (saw) na akamwambiya "Ewe Mtume wa Allah amka, usilale, Mola wako Anakuhitaji sasa hivi". Basi Mtume (saw) alipoamka, jopo la kundi la malaika likafika na kumlaza kwenye kitanda kingine kizuri sana mlemle ndani. Kisha wakamfanyia upasuaji wa kifua chake. Walipasuwa kifua cha Mtume (saw) halafu wakatowa nyongo na ghashi na uchafu wote. Baada ya kufanya upasuaji huo, malaika hao kwa wakati huo huo walishona kifua cha Mtukufu Mtume (saw), Wallahi haikuonesha kamwe dalili yoyote ya kupasuliwa kwake.

Baada ya upasuaji huo kufanyika, punde Buraku akajitokeza mbele ya Mtume (saw). Buraku ni kiumbe mwenye mbawa kama ndege, balini mwenye umbo la mnyama mwenye sura ya kibinadamu. Basi Jibril akamwambia Mtume (saw) kwa maneno yale yale ya mwanzo. Alimwambia "Ewe Muhammad Mola wako Anakusalimu. Yeye Anakuhitaji wende kwake haraka sana. Ametuletea Buraku huyu hapa tumpande ili twende chapu chapu". Jibril akamwambia Buraku, "Haya mchukuwe

*Endelea uk. 10*

# Kigoda cha Mwalimu Nyerere

Na Mahmood Hamsini Mubiru

Mambo matatu sitayasahau niliyaona katika tamasha la nne la Kigoda cha Mwalimu Nyerere. Tamasha hilo lilifanyika katika ukumbi wa Nkurumah Chuo kikuu cha Dar es salaam. Toka tarehe 13 hadi 14 mwezi Aprili 2012.

Kigoda cha Mwalimu kimeanzishwa ili kuenzi mchango wa Mwalimu katika kuharakisha ujengaji wa heshima ya binadamu. Wasomi kutoka Darimadari hukutana ili kuzungumzia matatizo yanayoikabili dunia yetu hii hususan bara la Afrika. Tayari wasomi maarufu akina Wole Soyinka, Samir Amiri wamekwisha toa mawazo yao katika tamasha hizo.

Mwaka huu walikaribishwa wanaharakati wawili kutoka Kenya, Micer Githae Mugo na Abdullatifu Abdallah waliozungumza juu ya wajibu wa Sanaa na mwandishi katika kuongoza ukombozi wa fikra na kupanua kanda zilizokombolewa.

Jambo la kwanza lililoniacha hoi bin taabani ni machapisho mapya ya vitabu vya Mwalimu Nyerere vilivyofanyiwa mapitio na Jenerali Ulimwengu. Machapisho hayo kimsingi ni juu ya ukombozi na kujitegemea - kujenga chetu. Lahaula! Kumbe vitabu hivi bado vinachapishwa na Oxford University Press. Inaumiza zaidi unapobaini kuwa Mwalimu Nyerere alianzisha Tanganyika Publishing House ili kuendeleza uchapishaji wetu wa vitabu vinavyotuhusu na matatizo yetu. Ni katika

*Endelea uk. 9*